**ATHARI ZA UDHANAISHI WA KIDINI KWA VIJANA KATIKA RIWAYA TEULE ZA *PARADISO* NA *KIDAGAA KIMEMWOZEA***

**MULI SOLOMON M.**

Mount Kenya University

**TASNIFU HII IMETOLEWA ILI KUTOSHELEZA BAADHI YA MAHITAJI YA SHAHADA YA UZAMILI KATIKA CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**CHUO KIKUU CHA MOUNT KENYA**

**JUNI 2024**

**UNGAMO NA IDHINI**

**Ungamo**

Tasnifu hii ni kazi asilia na wala haijawasilishwa na kutahiniwa katika chuo kingine kile.

Sahihi........ ..............................Tarehe ......................................

Muli Solomon M

MAKI/2020/64910

**Idhini**

Tasnifu hii imewasilishwa ili kutahiniwa kwa idhini yangu kama msimamizi aliyeteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Mount Kenya

Sahihi ...... .................Tarehe ................................................

Dkt. Jackline Njeri Murimi

Chuo Kikuu cha Tom Mboya

Homabay

Mount Kenya University

**TABARUKU**

Kwa mke wangu wa mtimani Angelina Lema,watoto wangu wa moyoni Joyce Mutheu na Josiah Muithi na kwa mama yangu  shujaa Veronica Muli.

Mount Kenya University

## SHUKRANI

Namshukuru Mwenyezi Mungu kwa siha njema aliyonikirimia nilipokuwa ninatayarisha kazi hii.Namshukuru msimamizi wangu Dkt. Jackline Njeri Murimi kwa  kunipa mawaidha ya dhati kwenye mchakato mzima wa kuandaa kazi hii.Mungu amzidishie  heri ili awe msaada kwa wanafunzi wengine.Shukrani ziende  Chuo Kikuu cha Mount Kenya kwa kuniruhusu kuendeleza masomo yangu  humo.

Nitakuwa mtovu wa shukrani nisipomshukuru mke wangu Angelina Lema,watoto wangu Joyce Mutheu na Josiah Muithi kwa uvumilivu wao wa kukosa starehe zinazowapasa nikigharamia masomo yangu.Isitoshe,namshukuru mama yangu mzazi Veronica Mutwa Muli kwa kuniadilisha hadi nikafikia miaka ya kufanya maamuzi.

Siwezi kuwasahau wahadhiri wangu wa idara ya Kiswahili  haswa Dkt. Alex Umbima Kevogo na Dkt Stanely Adika Kevogo kwa kunifundisha vyema hadi nikakienzi Kiswahili kwa  dhati.

Mwisho,ningependa kuwashukuru wanafunzi wazamili wenzangu;Josephene Kalumu,Wesley Oginge,Nancy Kavive,Winnie Atieno,Janet Waguyu,Grace Murugi,Edith Muthoni,Nancy Nkoroi,Faith Kathure na Jude Mukuta kwa kutangamana hadi tukafikia malengo tuliyokusudia elimuni.Nawatakia wingi wa heri katika maisha yenu ya usoni.

Mount Kenya University

## IKISIRI

Utafiti huu ulilenga kuchanganua sababu zilizowafanya baadhi ya vijana katika jamii kutamaushwa na dini kwa kurejelea riwaya ya John Habwe *Paradiso(*2005*)*na ya Ken Walibora *Kidagaa Kimemwozea(*2012*)*.Kwa mujibu wa Mbithi(2011),suala la imani katika Mungu ni nyeti na linatiliwa maanani na binadamu katika tamaduni mbalimbali kote duniani kama njia mojawapo ya kujaribu kutafuta majibu ya changamoto anazokubana nazo kila uchao.Katika jamii nyingi za Kiafrika,dini ni mfumo wa maisha ambapo kila mwana jamii alihitajika kushiriki.Hata hivyo,suala hili la kidini linaonekana kuwatamausha vijana wengi na kufifisha imani yao katika dini. .

Mtafiti alichunguza jinsi John Habwe na Ken Walibora wanavyoangazia udhanaishi wa kidini katika jamii.Ili Kukamilisha lengo hili kuu,malengo matatu mahususi yalizingatiwa.Malengo hayo ni pamoja na:kujadili vichocheo vinavyofanya vijana kutamaushwa na dini kwa mujibu wa riwaya teule za *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*,kutathmini athari zinazotokana na utamaushi wa kidini kwa mujibu wa riwaya teule za *Paradiso* na *kidagaa kimememwozea* na kuchanganua njia mbadala zinazoweza kutumiwa kuondoa utamaushi huu na kujenga imani ya umri wa vijana katika dini.

Utafiti uliongoza na nadharia ya Udhanaishi iliyoasisiwa na Mwanathiolojia kutoka Denmaki(1813-1855),Fredrick Nietzsche,Martin Heidegger,Gabriel Marcel na Karl Jaspers waliotokea karne ya 20 na Jean Paul Satre Mfaransa aliyetokea baada ya vita vya pili vya dunia.Mihimili yake ilisaidia mtafiti kufikia malengo ya utafiti. Mihimili mikuu ya nadharia ya udhanaishi ni pamoja na ;kutilia mkazo matatizo halisi yanayomsibu mwanadamu na kuwa na imani ya kijozi juu ya imani ya kuishi,inapalilia kutokuwepo kwa mungu na uumbaji wake wa ulimwengu,inatilia mkazo kuwa juhudi za mtu kujisaka au kujaribu kupambana na maisha huishia katika mauti,maudhui yake ni kama vile uhuru wa mtu binafsi kuweza kufikiri halafu kutoa jawabu lake.Nadharia husimulia taabu na kuchoka na hali ambazo husumbua yanayotatiza mwana wa adamu,nadharia hii inajadili mkengeuko,nadharia hii inachora taswira ya mateso anayopitia mwanadamu duniani,nadharia hii inatilia mkazo kuwa maisha yamejawa na utupu na kihoro hasa kuhusu siku za kesho.Maisha yamejawa na ubwege na huhakikisha binadamu kuwa mwisho wa maisha ni kifo.Nadharia hii ilifaa utafiti kwani ilitumika kueleza jinsi baadhi ya vijana waumini wanavyofasiri maisha jambo ambalo linawafanya watamaushwe na dini kila uchao.Nadharia hii ilitumika kupambanua ukweli wa je ni lipi ambalo baadhi ya vijana katika jamii wamejua hivi karibuni ambalo mababu zao hawakufahamu hapo awali?Utafiti ulifanyika maktabani kuliko na vitabu,majarida,matini na magazeti. Pia kulikuwa na shughuli za mtandaoni ambapo data ilipatikana kutokana na tasnifu zilizoandikwa kuhusu mkengeuko wa imani za kidini.Sampuli ya kimaksudi ilitumika katika kuteua riwaya *ya Paradiso na Kidagaa Kimemwozea*.Mbinu anuwai za kimaelezo zilitumika katika kuchambua data na kuwasilisha matokeo kwa lugha ya nadhari kuambatana na malengo ya utafiti.Maarifa yaliyopatikana katika utafiti huu yatakuwa na mchango mkubwa katika maarifa yaliyopo kuhusu vijana na masuala ya dini katika jamii.Mapendekezo ya utafiti huu yatasaidia viongozi wa madhehebu tofauti katika harakati za kujenga upya maadili yanayozidi kumomonyoka miongoni mwa vijana. Utafiti huu utatumika na wasomi,waandishi na wataalamu wengine katika kutafitia masuala yanayohusiana na dini.Isitoshe,utafiti huu utatumika kama hazina ya marejeleo ya siku za usoni.

# ABSTRACT

This research aimed at analyzing the reasons why the generation of current youth has been dislussioned by the religion basing the urguments in the two novels authored by John Habwe and Ken Walibora respectively.The issue of faith in" God" is critical and has been forwarded by humans of different cultures all over the world as one of the methods used to give solutions to challenges which humans come across daily.in many African societies,religion was a system which demanded every member of the society to participate in.However, this issue of religion has been recently disappointed many youths and lowered ethuasism in its practice.To accomplish this main objective,three specific objectives have been reviewed.These objectives include;to discuss reasons which has discouraged the youth and diverted them from religion, to evaluate the effects of the religious ignorance among the youth in the community, to analyze alternative methods which can be used to rebuild religious faith among the youth.This research was guided by the theory of Existentialism and that of Absurd where their foundations helped the researcher achieve the goals of the research.The main foundations of the theory of existentialism include; platform on the real challenges that humans face daily and build a dream of faith to live,it propagates the absence of God as sore creator of universe, this theory of raises the concerns that all the efforts of humans to know the real meaning of life leads to death,the themes of this theory are the personal freedom and the power to think and make personal decisions in life,the theory analyzes how daily challenges affects the human life,it also discusses the theme of doubt.This theory draws the whole picture of human life and challeges he faces daily.The theory still analyses how life is full of void and fear more so of facing the future,the theory analyses how human life is full of absurdness and then assures this human that the end human life is death.The use of this theory was relevant to the study since it was used to explain how some youth believers see life and how their view makes them to be fed up by religion day in day out.This theory was used to evaluate the truth on what has been known by some members of youth in the community which was not known by their grants.In collecting data, the research used library where books, magazines,journals,papes and unpublished thesis related to the topic of study.Again online research where basic data was obtained from thesis written about the religion was utilized.The online research gave information on data that explains about the community and beliefs.Purposeful sampling was employed in this study.Deceptive methods in analyzing the data and presenting it in the prose and clear language in the line with research objectives were used.The knowledge contained in this research will be a contribution to existing knowledge about the issues of the of the youth in matters of religion in the society.The recommedations of this research will add the knowledge to different categories of members of the society and more so religious leaders in rebuilding the morals of the youth which are degrading time to time.This research will be used by scholars,authors and other specialists in the issues related to religion. Moreover,this research will act as rich source of references in the future.

Mount Kenya University

**UFUPISHO**

**BBC-** British Broadcasting Cooperation

**WHO-** World Health Organisation

**TUKI-** Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili Nchini

**UN-** United Nations

**USA-** United States of Amerika

Mount Kenya University

## YALIYOMO


**UNGAMO NA IDHINI** ........ i
**Ungamo** ........ i
**Idhini** ........ i
**TABARUKU** ........ ii
**SHUKRANI** ........ iii
**IKISIRI** ........ iv
**ABSTRACT** ........ v
**UFUPISHO** ........ vi
**SURA YA KWANZA** ........ 1
**1.0 Utangulizi** ........ 1
**1.1 Usuli wa Utafiti** ........ 1
**1.2 Tatizo la Utafiti** ........ 2
**1.3 Malengo ya Utafiti** ........ 3
**1.4 Maswali ya Utafiti** ........ 3
**1.5 Sababu za Kuchangua Mada** ........ 4
**1.6 Umuhimu wa Utafiti** ........ 5
**1.7 Upeo wa Mipaka ya Utafiti** ........ 5
**1.8 Maelezo ya Istilahi Zilizotumika** ........ 6
**1.9 Hitimisho** ........ 6
**SURA YA PILI** ........ 7
**MWAUO WA MWANDISHI** ........ 7
**2.0 Utangulizi** ........ 7
**2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada** ........ 7
**2.2 Msingi wa Nadharia** ........ 15
**2.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi** ........ 17
**2.2.2 Ubwege** ........ 17
**2.2.3 Sifa za Ubwege** ........ 18
**2.3 Hitimisho** ........ 19
**SURA YA TATU** ........ 20
**MBINU ZA UTAFITI** ........ 20
**3.0 Utangulizi** ........ 20


Mount Kenya University

**3.1 Muundo wa Utafiti** ..... 20
**3.2 Wango la Utafiti** ..... 20
**3.3 Uteuzi wa Sampuli** ..... 20
**3.4 Eneo la Utafiti** ..... 21
**3.5 Ukusanyaji wa Data** ..... 21
**3.6 Uchanganuzi wa Data** ..... 22
**3.7 Maadili ya Utafiti** ..... 22
**3.8 Hitimisho** ..... 23
SURA YA NNE ..... 24
**UCHANGANUZI WA DATA NA UFASIRI WA MATOKEO YA UTAFITI** ..... 24
**4.0 Utangulizi** ..... 24
**4.1 Historia fupi ya John Habwe** ..... 24
**4.2 Historia fupi ya Ken Walibora** ..... 25
**4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Paradiso*** ..... 26
**4.4 Muhtasari wa Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*** ..... 28
**4.5 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti** ..... 30
**4.5.1 Sababu za Kidini Zinazowatamausha Vijana katika Riwaya Teule za Paradiso na Kidagaa Kimemwozea.** ..... 30
**4.5.2 Mipango ya Kando baina ya Waumini.** ..... 30
**4.5.3 Mifarakano ya Madhehebu** ..... 32
**4.5.4 Ulaji na Matumizi Mabaya ya Zaka, Sadaka na Matoleo** ..... 33
**4.5.5 Maabadi kuwa Mali ya Familia** ..... 34
**4.5.6 Biashara kwa Jina la Mungu.** ..... 35
**4.5.7 Ufisadi Miongoni mwa Viongozi wa Dini.** ..... 36
**4.5.8 Injili Kuwa Chombo cha Kujitajirisha** ..... 38
**4.5.9 Wahubiri Kuishi Maisha ya Starehe na Anasa kwa Gharama ya Matoleo na Misaada.** ..... 39
**4.5.10 Viongozi wa Kidini na Waumini Kuhusishwa na Uganga na Mapepo** ..... 40
**4.5.11 Unafiki wa Matendo Miongoni mwa Wanadini** ..... 41
**4.6 Athari za Utamaushi wa Kidini kwa Vijana** ..... 43
**4.6.1 Vijana Kuchoshwa na Utaratibu wa Maabadani.** ..... 43
**4.6.2 Vijana wa Kike Kukataa Kuolewa na Wahubiri.** ..... 43
**4.6.3 Vijana Kushuku Uwezo wa Mungu.** ..... 45
**4.6.4 Vijana Kukataa 'Kuokoka' na Kuingia kwa Anasa.** ..... 46
**4.6.5 Vijana Kuzinduka na Kuuliza Maswali Kuhusu Dini Hadharani.** ..... 47
**4.6.6 Vijana Kuacha Kuhudhuria Ibada.** ..... 49

Mount Kenya University

**4.6.7 Vijana Kuwa na Ukakamavu wa Kudharau Watumishi wa Mungu Peupe.**..................50
**4.6.8 Vijana Kukataa Kazi ya Mungu Peupe.** ..............................................................51
**4.6.9 Vijana Kutafuta Miungu na Ibada Zingine.**.......................................................52
**4.7 Mapendekezo ya Waandishi John Habwe na Ken Walibora ya Kukabiliana na Udhanaishi wa Kidini kwa Vijana**…………………………………………………………………………………………
**4.8 Hitimisho**......................................................................................................56
**SURA YA TANO** ..............................................................................................57
**MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO**.......................................................57
**5.0 Utangulizi**....................................................................................................57
**5.1. Muhtasari wa Utafiti**......................................................................................57
**5.2 Mapendekezo ya mtafiti.** ..................................................................................53
**5.3 Hitimisho**......................................................................................................61
**MAREJELEO** ..................................................................................................63
**Kiambatisho I:Barua ya idhini ya Chuo.(ERC)**.......................................................66
**Kiambatanisho II: Barua ya Idhini(NACOSTI)** .......................................................69

Mount Kenya University

## SURA YA KWANZA

### 1.0 Utangulizi

Kwenye sehemu hii mtafiti alifafanua usuli wa mada,tatizo la utafiti,malengo ya utafiti, maswali ya utafiti,sababu za kuchangua mada, umuhimu wa utafiti,upeo na mipaka ya utafiti pamoja na maelezo ya istilahi ya zilizotumika.

### 1.1 Usuli wa Utafiti

Kulingana na Cames(1984),udhanaishi ni falsafa inayoshughulikia maswali kuhusu maisha ya mwanadamu.Kwa jumla,ni mtazamo unaokagua kwa mapana nafasi ya mwanadamu katika ulimwengu anamoishi.Vile vile,ni falsafa inayoelezea mahusiano yaliyomo kati ya mwanadamu na Mungu na ikiwa mwanadamu huyu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu au la.Taabu na matatizo anayokumbana nayo mwanadamu zinamfanya kuwa na maswali chungu nzima kuhusu maisha haswa juu ya masuala ya uwepo wa maadili na kiroho.Kwa mujibu wa Mark Sanchez(2021),dini ni mfumo wa imani,mila na alama zilizoanzishwa karibu na wazo la uungu au kutoka takatifu.Dini ni mafundisho yaliyoundwa na seti ya kanuni,imani na mazoea anazoenzi binadamu anapokosa suluhu mwafaka kuhusu hali nyeti anazokutana nazo maishani. Baada ya zama za giza,mwanadamu alianza kujisatiti kutafuta suluhu la maisha kwa nyanja tofauti ikiwepo dini.

Dini ni neno linalopatikana uarabuni ‘Diin’ linalomaanisha ‘imani ya umoja wa mwenyenzi ‘Mungu’,desturi,tabia au mazoea.Kwa jumla neno hili husisitiza maana ya mwanadamu kuitambua nguvu kubwa kumliko na ambayo inautawala ulimwengu mzima na haswa Mungu au Miungu ya mtu binafsi kama mwongozo wa kiroho,kiimani na kiibada.Dini ndio mafundisho ambayo huunganisha sana mwanadamu na Mungu au Miungu,yaani ni hatua na athari za kuunganisha tena Mungu na wanadamu.Neno dini linaweza kutumika kiishara kuashiria

Mount Kenya University

shughuli au wajibu unaofanywa kila wakati huku masharti fulani yakizingatiwa.Mifano ya dini duniani ni ile ya Kikristo iliyo na waumini bilioni 2.1,ile ya Kisilamu yenye waumini bilioni 1.9 pamoja na ya Kibudha iliyo na waumini bilioni 1.6. Kulingana na vitabu vya kihistoria vya dini,makundi ya kidini yaliyoimarika yalionekana kwa mara ya kwanza baada ya machimbuko ya kazi na ukuzaji wa kilimo ambapo wanadamu walitumia wakati mwingi kutazama maumbile. Dini za *Neolithic* ziliundwa karibu na vitu vitatu;hekalu,kuhani na dhabihu(matoleo) ambayo pia ni kielelezo cha utambuzi wa takatifu na unajisi.

Kazi ya dini ni kuimarisha mfumo wa maadili yanayohusu mshikamano wa kikundi cha jamii kulingana na mradi wa kawaida na kuunda kiwango fulani cha kuridhika kiroho kupitia imani kushinda kuteseka na kufikia furaha.Dini zote zina misingi ya kihistoria zilizoitwa hadithi za uwongo zikieleweka kama hadithi zinazoelezea asili ya maisha,kuhalalisha hali yake na makadirio yake ya baadaye.Isitoshe,kila aina ya dini inaungwa mkono na mikondo tofauti ya mawazo ambayo hujaribu kueleza dhana ya wanadamu pamoja na umuhimu wao wa kuwa ulimwenguni. Katika tamaduni zilizo na maandishi,dini zinategemea maandishi ya asili takatifu ambayo huleta wafuasi wao karibu na jamii moja ya kiroho.Kwa mujibu wa vitabu vya kihistoria,imani ya dini za kigeni zilisambazwa maeneo mengi ya dunia na Wazungu kutoka Bara la Ulaya pamoja na Waarabu kutoka Mashariki ya mbali kabla na baada ya zama za giza..

### 1.2 Tatizo la Utafiti

Katika karne ya 21 na haswa baada ya ujio wa kipindi cha utandawazi,kumekuwa na ugumu kwa wazazi na haswa wazee waliokomaa kwenye masuala ya kidini kukielekeza kizazi cha vijana wa karne hii katika masuala ya kiimani.Waandishi wa kazi za fasihi wa viwango tofauti wamekuwa kwenye msitari wa mbele kuangazia sababu zinazotamausha vijana katika maisha.Vile vile,waandishi husika wamekuwa wakitoa mapendekezo mwafaka ya kuangazia suala hili nyeti la utamaushi linalotishia kuangamiza kizazi cha vijana wa leo.Utamaushi wa maisha miongoni mwa vijana umeanza kukita mizizi katika nyanja tofauti zikiwemo elimu,familia na ndoa,



Mount Kenya University

unadhifu kwa jumla,uwajibikaji na maadili kwa jumla.Masuala haya na mengine yamekuwa yakiangaziwa katika kazi tofauti za fasihi na waandishi waliobobea na wale chipukizi.Lengo lao huwa kuyaweka wazi na kutoa mapendekezo yanayoweza kuzingatiwa kupunguza hali hii ya utamaushi.Katika utafiti huu,mtafiti aliangazia riwaya mbili zilizotungwa na waandishi waliobobea katika karne ya ishirini na moja.Alijikita katika riwaya ya John Habwe *Paradiso* (2005) na ile ya Ken Walibora *Kidagaa Kimwemwozea (*2012). Mtafiti alikusudia kuangazia sababu za vijana kutamaushwa na dini,athari za utamaushi wa kidini kwa jamii za vijana hawa pamoja na njia mwafaka za kukabiliana na utamaushi wa kidini kwa vijana kwa mujibu wa riwaya hizi mbili teule.

## 1.3 Malengo ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na malengo yafuatayo;

1. Kujadili vichocheo vya utamaushi wa kidini kwa vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya teule ya *Paradiso* ya John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora.
2. Kutathimini athari za utamaushi wa kidini kwa vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya teule ya *Paradiso* ya John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora.
3. Kuchanganua njia mbadala za kupambana na utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya teule ya *Paradiso* ya John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora.

## 1.4 Maswali ya Utafiti

Utafiti huu uliongozwa na maswali yafuatayo;



Mount Kenya University

1. Je,ni nini kinachochea utamaushi wa kidini kwa vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya teule ya *Paradiso* ya John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora?
2. Je,utamaushi wa kidini kwa vijana katika jamii una athari zipi kwa mujibu wa riwaya teule ya *Paradiso ya* John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora?
3. Je,jamii inaweza kutumia njia zipi mbadala katika kupambana na utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya teule ya *Paradiso* John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora ?

## 1.5 Sababu za Kuchangua Mada Hii

Kazi maridhawa katika fasihi huangazia masuala tofauti yanayoathiri jamii kwa jumla kama vile uozo,maadili,dhuluma,usawa,magonjwa na kadhalika.Kazi maridhawa zinazoshughulikia masuala ya jamii huelezea namna jamii inavyokubana na matatizo ya kila aina yanayozidi kufisha vijana moyo na kufanya maadili yao yamomonyoke siku baada ya siku. Mojawapo wa taasisi zilizoenziwa na jamii kushughulikia mmomonyoko wa maadili miongoni mwa vijana ni ile ya dini.Watafiti wengi wamejikita kwa upana kuangazia namna vijana wanavyokata tamaa maishani na kujitosa kwenye lindi la maangamizi ya kila aina bila kujali kesho yao. Kwa vile mafundisho ya dini yaliweka misingi mizuri kwa maadili ya vijana wa jamii ya mwanadamu,kumeshuhudiwa visa ambavyo vijana wamezidi kutamaushwa na taasisi hii ya dini. Daima fasihi ni kioo cha jamii na licha ya kazi za fasihi kupalilia dini kama kiungo cha kufundisha vijana maadili,kazi hizi hazijashughulikia sababu za vijana kuzidi kutamaushwa na taasisi hii ya dini jinsi siku zinavyosonga. Kwa kutilia maanani mchango wa taasisi ya dini katika kufundisha vijana maadili,kuna haja ya kuangazia sababu zinazofanya vijana wengi watamaushwe na dini katika jamii. Katika utafiti huu,mtafiti alichuguza sababu zinazofanya vijana kutamauka kidini. Kupitia utafiti huu,mtafiti alinuia kuonyesha changamoto za kidini zinazowakumba vijana na hivyo kuwatamausha.Vivyo hivyo,mtafiti alinuia kuangazia jinsi suluhu mwafaka la utamaushi huu linavyoweza kupatikana.

Mount Kenya University

### 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Utafiti huu utasaidia kujenga maadili miongoni mwa vijana yanayozidi kumomonyoka kila uchao na kupunguza mafarakano wazee wanapojaribu kuwarudisha vijana kwa maadili bora yaliyohasisiwa na mababu zao katika masuala ya dini.

Vile vile utafiti huu utawafaa wanafasihi na hasa walimu wa fasihi kwa kuelewa zaidi maudhui ya dini yanayozidi kupanuka kila uchao katika fasihi na Kiswahili kwa jumla. Pia utafiti huu utaaangazia mbinu za kupunguza kiwewe kwa viongozi wa madhehebu tofauti kwa hofu kuwa masuala ya ibada na dini yatafifia baada ya kizazi cha wazee walio na umri wa miaka 60 na zaidi kufikia kikomo chao.

Aidha,utafiti huu utatumika kama mapendekezo ambayo yanaweza kusaidia viongozi wa madhehebu tofauti kuibuka na njia za kushughulikia suala la upungufu wa waumini vijana katika jamii.Isitoshe,utafiti huu utachangia katika ufundishaji wa Kiswahili na haswa fasihi. Utasaidia kubainisha jinsi waandishi tofauti wanavyoshughulikia suala nyeti la utamaushi wa kidini katika kazi zao. Mwisho,utafiti huu utatumika kama marejeleo kuzidisha maarifa kwa wanafasihi katika kuhakiki kazi tofauti zinazoshughulikia utamaushi wa kidini katika jamii.

### 1.7 Upeo wa Mipaka ya Utafiti

Suala la utamaushi wa kidini limesheheni katika jamii.Kuna riwaya,tamthilia na hadithi fupi maridhawa za Kiswahili zinazoangazia suala nyeti la utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana katika jamii.Licha ya utele huu wa maandishi,mtafiti alichangua riwaya mbili pekee ili kuhakiki jinsi watunzi wake walivyoangazia suala nyeti la utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana katika jamii.

Mtafiti alishughulikia vijana waliotamauka kimatendo na kimaadili na kuonyesha jinsi vijana hawa wanavyozidi kukatishwa tamaa na dini na kusambaza mawazo yao yanayopinga masuala ya kidini kila uchao. Mtafiti alitumia njia ya kimakusudi kuteua riwaya ya John Habwe *Paradiso* (2005) na ya Ken Walibora *Kidagaa Kimemwozea*(2012) kwani zilimfaa zaidi katika utafiti

wake. Kazi hizi zinaafiki hali ilivyo sasa kwani zimeandikwa katika karne ya 21 na hivyo basi zilimsaidia kufikia malengo yake.

### 1.8 Maelezo ya Istilahi Zilizotumika

- **Dini** – ni mkusanyiko wa imani za mwanadamu.
- **Ibada** – ni tendo la kumwabudu Mungu
- **Maadili** – ni mafundisho mema, yanayotolewa kwa ajili ya kufundisha vijana (mwana wa kiume au kike) hadi umri wa kubalehe. Aliye na umri wa miaka 18 hadi 35 (kulingana na katiba ya kenya 2010)
- **Maabadi**- mahali wanamokutana waumini kufanya ibada kulingana na dini na imani zao.
- **Ombwe** – uwazi usio na kitu chochote.
- **Madhehebu** - ni kikundi cha dini fulani chenye mwelekeo fulani na kikundi kingine cha dini hiyohiyo moja
- **Ukengeushi** – hali ya kwenda kombo, ni upotoshi wa kitu, mtu au jambo kuenda bila kufuata kanuni zinazofaa kufuatwa yanatokana na kukata tamaa.
- **Utamaushi**- hii ni hali ya kukata tamaa maishani;yaani kukosa ladha na matumaini maishani na kuacha jaala ichukue mkondo wake.

### 1.9 Hitimisho

Katika sura hii mtafiti alishughulikia usuli wa utafiti,tatizo la utafiti,malengo ya utafiti pamoja na maswali ya utafiti.Vile vile,aliangazia sababu za kuchangua mada,umuhimu wa utafiti,upeo na mipaka ya utafiti pamoja na maelezo ya istilahi zitakazotumika katika utafiti.

Mount Kenya University

# SURA YA PILI

# MWAUO WA MWANDISHI

## 2.0 Utangulizi

Sura hii iliangazia maandishi tofauti yaliyoandikwa kuhusu mada hii. Kazi hizi tangulizi zina umuhimu mpana kwa mtafiti yeyote yule kwani zilimwelekeza kupekua taaluma iliyofichwa na kuitambua pengo lililopo ndani yake. Kwenye sehemu hii, mtafiti amepanga kazi yake kisehemu.Sehemu ya kwanzainahusu maandishi ya kazi zilizotangulia ilhalii ile ya pili inaangazia msingi wa nadharia.

## 2.1 Yaliyoandikwa Kuhusu Mada

Mugha(1999),huku akimuangazia mwandishi Kezilahabi,anajadili jinsi mwandishi huyu tajika alivyotamaushwa na mazingira ya shule alikopelekwa haswa ya kiseminari ambapo alishindwa kufuzu na kuwa padri. Vile vile Mugah anaeleza jinsi Kezilahabi alivyotamaushwa kwa kuona serikali mpya ya mtu mweusi ikimkadamiza mwananchi wake na kumsababibishia mateso zaidi. Kazi ya Mugah ilifaa mtafiti kwani inajadili kuhusu utamaushi unaojikita kwenye mazingira fulani;yaani yale ya shuleni na ya uongozini. Tofauti ya kazi ya Mugha na ya mtafiti ni kuwa kazi ya mtafiti ilijikita kwenye mazingira yote kwa ujumla kwa kuangazia utamaushi wa kidini miongoni mwa waumini vijana hawa ili kuibuka na sababu za utamaushi huu,athari zake kwa jamii wanamotoka pamoja na mapendekezo ya kukabiliana na hali hii ya utamaushi wa kidini.

Kulingana na kazi ya Magare (2002) katika tasnifu yake ya uzamili anasema kuwa dini huwa kifaa cha kuongoa mwana wa Adamu anayetishwa na dunia kwa kumtumainisha kuwa Muumba ameandaa mahala pengine pazuri kwa ajili yake. Kulingana na Magare ni kuwa binadamu anapaswa kukabiliana na dunia aliyomo kwani dini na imani haziwezi kusuluhisha matatizo yake ya kila siku. Utafiti wa Magare umeshughulika binadamu kwa jumla na jinsi imani kuhusu mahali pema alipotengenezewa na" Mungu" inavyozidi kufifia kwani

Mount Kenya University

anazidi kutaabika zaidi. Katika utafiti huu,mtafiti alijikita kwa kipengele cha vijana ili kubaini sababu zinazowafanya watamaushwe na masuala ya kidini,athari za utamaushi huu kwa jamii zao pamoja na mapendekezo mwafaka ya kupambana na utamaushi huu.

Cooper(2004) anasema kuwa binadamu hukutana na matatizo halisi yanayomsibu mtu binafsi katika hali ya kukwepa imani ya kijonzi juu ya maana ya maisha. Anasema kuwa jitihada za binadamu za kujitafutia ukweli wa maisha kila mara hutiwa kikomo na mauti. Kazi ya Cooper inafafanua kuwa binadamu hutamaushwa na matatizo anayokutana nayo kila uchao. Kazi hii ilikuwa na manufaa kwa mtafiti kwani inazungumzia mojawapo wa kiini cha utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana;yaani matatizo anayokubana nayo. Mtafiti alinuia kupambanua matatizo haya yanayowafanya vijana watamaushwe na dini kwa undani wake,athari za utamaushi huu kwa jamii wanamotoka vijana hawa na kisha mapendekezo mwafaka ya kukabiliana na ongezeko la utamaushi huu wa kidini.

Mose,E(2005) katika utafiti wake anajadili jinsi binadamu anavyotamaushwa na kunyong'onyezwa na suala la kifo.Kulingana na Mose,kifo humfanya binadamu kuona jinsi maisha yalivyojazwa na utupu jambo ambalo humkosesha binadamu tamaa ya kuishi. Kazi hii ilikuwa na muhimu mkubwa kwa ile ya mtafiti kwani iliangazia namna binadamu anavyotamaushwa na kifo.Kazi hii ina utofauti kwa kiasi na kazi ya mtafiti kwani udhanaishi aliojishughulisha nao haujatokana na kifo ila ulitokana na suala nyeti la kidini miongoni mwa vijana kwa lengo la kuelewa zaidi sababu za udhanaishi huu wa kidini,athari zinazoshuhudiwa katika jamii kutokana na utamaushi huu pamoja na mapendekezo kabambe ya kupunguza utamaushi huu.

Gakii (2006) ameshughulikia udhanaishi katika riwaya ya *Kichwamaji* katika tasnifu yake ya uzamili.Akiangazia udhanaishi kwenye diwani ya *Kichwamaji*,Gakii anasema udhanaishi katika



Mount Kenya University

diwani hii unatokea pale mwandishi wa riwaya hii Kezilahabi anaonyesha kuwa kuna wanaoamini kuwa Mungu yupo na wakati huo huo kuna wale ambao hawana imani katika Mungu. Mgawanyiko huu wa dhana inayohusiana na Mungu inajitokeza wazi kupitia kwa usemi wa kazimoto kwamba mwanadamu atasali wakati huo huo wengine wanapiga kelele kwamba hakuna Mungu (uk140).Hata hivyo kupitia kwa kazimoto na Manase,mwandishi anadadisi kuwako kwa Mungu kinyume na wakristo ambao huamini kuwa Biblia ni neno la Mungu, kazimoto anaona kuwa Biblia ni kitabu cha zamani ambacho labda kimepitwa na wakati. " Nilianza kujiuliza kwa nini nilisoma kile kitabu cha zamani –Biblia" (uk 50). Aidha anatoa maoni yake kwa wazee kuwa anashuku kuwepo kwa Mungu. Anasema "huenda hakuna Mungu" (uk 59)Kutilia shaka kuwepo kwa Mungu kunaendelezwa na ndoto ya Kalia ambayo anaota akiwa mbinguni lakini haoni Mungu wala watu waliokuwa motoni. Jambo hili linatuonyesha kuwa dhana ya peponi au Jehanamu haina mashiko. Hoja hii inatiliwa mkazo na kazimoto ambaye anashuku kuwepo kwa Jehanamu anaposema "shetani naye ana bahati nzuri..... nikifikiria kwamba wanawake wazuri wengi huenda motoni ... kama kuna moto na shetani huwafaidi (uk 114) . Kazi hii ilitufaa kwani msomi Gakii ameshughulikia imani za kijonzi zinazotamausha wahusika wa umri tofauti. Hii ni tofauti na kazi ya mtafiti ambayo ilinuia kushughulikia masuala halisi ya kidini yanayotamausha vijana wa jinsia zote huku akiangazia sababu za utamaushi huu,athari zake kwa jamii pamoja na njia mbadala zinazoweza kupunguza utamaushi huu.

Mbatiah(2008)akiangazia riwaya ya *Dunia Uwanja wa Fujo*,anadai kuwa maisha ya mwanadamu ni vurumai tupu ambayo huletwa ulimwenguni na watu fulani katika nyakati mbalimbali za kihistoria. Anadai kuwa mwanadamu ni kiumbe dhaifu kisichoweza kuudhibiti ulimwengu na kuwa juhudi zozote anazofanya binadamu ili apate furaha zinasindwa. Hali hii inamfanya binadamu atamauke zaidi kwani hana uwezo wa kudhibiti mazingira yanayomzunguka. Kazi ya Mbatia inajadili jinsi mwanadamu kwa jumla alivyoshindwa

Mount Kenya University

kuudhibiti ulimwengu anamoishi kwa sababu ya udhaifu wake. Kazi hii ya Mbatiah ilikuwa na umuhimu mkubwa kwa kazi ya mtafiti kwani inajadili kwa jinsi binadamu alivyotamaushwa na ulimwengu anamoishi.Tofauti ya kazi ya Mbatiah na ya mtafiti ni kuwa mtafiti hakuangazia utamaushi unaosababishwa na ulimwengu kwa jumla ila aliengemeza kazi yake kwa masuala ya kidini na jinsi dini inavyoshindwa kudhibiti akili za vijana na kuwafanya wakate tamaa kwa kukosa suluhu ndani yake huku akilenga zaidi kufafanua sababu za utamaushi huu,athari zake kwa jamii na mapendekezo mwafaka ya kuleta suluhu ya hali hii tata.

Kulinganana na ripoti ya Jesse,Wafula na King'ei (2011),dini inatumiwa kama kipengele cha utawala wa ulimwengu unaotawaliwa utandawazi ili mataifa tajiri yaendelee kuhifadhi na kuendeleza utajiri,biashara na manifesto ya kiuchumi na utawala huku mataifa yanayoendelea na ya kimasikini yakizidi kupotelea kwa dini mbalimbali kwani hawana suluhu.Wataalamu hawa wanajadili namna utandawazi unavyozidi kutajirisha mataifa yaliyoendelea kinyume na wanaoamini dini kama mwokozi wao ambao wanazidi kumasikinika na kutamausha zaidi na hali ya uchumi kwenye mataifa yao. Kazi ya wataalamu hawa ilikuwa na umuhimu kwa kazi ya mtafiti kwani ilijadili jinsi raia wengi wanavyotamaushwa na hali ya kuweka imani yao yote kwenye dini badala ya utandawazi. Hii ni kinyume na kazi ya mtafiti ambayo iliepuka utamaushi unaozalishwa na kukua kwa utandawazi kwa raia wote kwa jumla na badala yake kujikita kwenye kipengele cha vijana huku akitafitia sababu zinazofanya vijana hawa watamaushwe na dini,athari za utamaushi huu katika jamii wanapotoka vijana hawa na kisha njia mwafaka za kushughulikia hali hii.

Katika tasnifu yake Ng`etich,K(2011) anasema kuwa dini ni chombo cha kudhulumu waumini kisaikolojia,kiuchumu,kifamilia, kiwakati na kiakili kwa jumla. Ingawa dini ni chombo muhimu cha kupalilia maadili na umoja wa kijamii,baadhi ya waumini wanaitumia kudhulumu wenzao. Hii inasikitisha kwani binadamu kwa mapana hana nafasi ya kupinga kinachohusiana na"

Mungu".Utafiti huu umeshughulikia dhuluma za kidini zinazowatamausha waumini kwa jumla ila kwa upande wa mtafiti aliagemea vijana pekee ambao haswa sio lazima watamaushwe na dhuluma za kidini mbali unafiki uliopo kwa jumla huku mtafiti akizama zaidi kuelewa sababu za utamaushi huu,athari zake kwa jamii za vijana athiriwa  na njia mbadala zinazoweza kupambana na hali hii.

Ogutu (2013) katika tasnifu yake ya uzamili anasema kuwa mabadiliko ya kidunia kuhusu masuala ya kidini yanabadilisha masuala ya kindoa.Anasema kuwa sehemu za ibada hazistahili kuachwa nyuma na kubadilika huku., la sivyo maabadi haya yatapoteza vijana hawa katika madhehebu yao.Kazi hii ya Ogutu inaangazia mabadiliko ya dunia kama kigezo kinachotia waumini kiwewe wanapokosa kuona mabadiliko katika madhehebu yao na hivyo kukata tamaa ya kuenzi masuala ya kidini. Kazi hii ya Ogutu ilifaa utafiti huu kwani inajadili jinsi mabadiliko ya dunia yanavyotamausha vijana kwa jumla huku madhehebu yao yakibakia mle mle.Utofauti wa kazi ya Ogutu na ya mtafiti ni kuwa yeye aliangazia kipengele cha waumini vijana kutamaushwa na dini,athari zinazoshuhudiwa kwenye jamii kutokana na utamaushi huu pamoja na mapendekezo mwafaka ya kushughulikia hali hii ya utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana hawa.

Rono (2013) katika tasnifu yake,alihakiki utamaushi wa wahusika katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea.* Rono anadai kuwa wahusika Amani na Imani wanatamaushwa na hali ya maisha iliyoko kwa familia zao na hivyo kukata tamaa na kuamua kutoroka nyumbani na kwenda wasikokujua. Amani anaamua kufunga safari ya kwenda asikokujua ilhali Imani ana mpango wa kwenda kujitosa ndani ya ziwa Mawewa. Walikuwa wametamauka kiasi cha kuachia jaala nafasi iwapeleke itakako. Katika kazi hii wahusika wakuu ambao ni vijana wametamaushwa na hali nzito inayokuba familia zao kulikokuwa na matumaini na hivyo kukata tamaa na kuamua kutoroka makwao. Mapitio ya kazi hii yalikuwa na umuhimu kwa mtafiti kwani inajadili

Mount Kenya University

utamaushi wa kifamilia unaowaathiri vijana kiasi cha kuwafanya kutoroka makwao . Kazi hii licha ya kuangazia vijana, imejikita kwenye mazingira ya nyumbani ilhali mtafiti alijikita kwenye mazingira ya vijana wawa hawa kwenye mazingira tofauti yanayolingana na imani na dini huku akizama zaidi kuangazia sababu na athari za utamaushi huu,athari zake kwa jamii pamoja na mapendekezo mwafaka ya kushughulikia utamaushi huu miongoni mwa vijana.

Odongo,O(2014) katika tasnifu yake,alihakiki utendi wa *Mwanakupona* unaoshikilia kuwa kifo ni afueni zaidi kwa binadamu kuliko maisha yanayompa dhiki chungu nzima.Akiangazia mhusika Martha katika utendi wa *Mwanakupona*,anabaini kuwa kifo huwa dawa ya kumwepusha na kumpoza mtu machungu yanayoletwa na maisha.; ni mfariji mwema kwa mtu mwenye dhiki(uk 55).Msomi Odongo anasisitiza kuwa dhiki za kiujumla anazokumbana nazo binadamu ndizo zinazomkatisha tamaa ya kuishi hadi kuamua kujiua.Kazi hii ni ya manufaa kwa mtafiti kwani inapanua mojawapo wa athari zinazotokana na utamaushi wa maisha;yaani athari ya kujiua.Utafiti aliojishughulisha nao mtafiti ulinuia kuangazia athari nyingi za utamaushi kwa kuengemea kipengele cha imani ya kidini miongoni mwa vijana,athari za hali hii kwa jamii pamoja na njia mwafaka zinazoweza kutiliwa maanani kukabiliana na hali hii ya utamaushi wa kidini.

Makoyo (2014),katika tasnifu yake ya uzamili,anajadili jinsi elimu ya Kenya anavyotamausha wasomi kwa kuegemezwa kwenye dini ya Kikristo.Kwa mujibu wa Makoyo ,kuamini huku kunawafanya watu washindwe kujitegemea kwa sababu wanahofia kufanya maamuzi muhimu maishani mwao kwa hofu ya kupata ghadhabu kutoka kwa Mungu. Hali hii inamfanya mwanadamu kujiona kama kiumbe kisicho na akili ya kufanya maamuzi yoyote na hivyo kumkatisha tamaa zaidi. Kazi hii ya Makoyo ni muhimu kwa mtafiti kwani inarejelea mada ya utamaushi miongoni mwa wanajamii.Tofauti ya kazi hii ya Makoyo ni muhimu katika utafiti kwani tunapata jinsi elimu ya taifa la kenya inavyokatisha wasomi tamaa. utafiti huu uliepuka

utamaushi unaosababishwa na elimu na kujikita kwa ule unaosasababishwa na masuala ya kidini kwa vijana,athari za utamaushi huu kwa jamii wanamotoka vijana hawa na njia zinazoweza kuangaziwa kuleta suluhu mwafaka za utamaushi huu ili kujenga upya imani ya kidini kwa vijana.

Nyamemba,R(2016) katika tasnifu yake ya uzamili anasema kuwa vijana wanapokosa kupata matarajio waliyokuwa nayo kwa nyanja mbalimbali kama vile elimu na ajira,wengi wao hutamauka na kuamua kujitosa kwenye dawa za kulevya za kila aina zikiwemo bangi,ugoro na singara.Hali hii imewafanya wengi wao kukosa kujukumika katika jamii.Kazi hii ya Nyamemba inafafanua kuwa vijana wengi hukatishwa tamaa na ukosefu wa masuala ya kiuchumi kama vile elimu na ajira na hivyo kukata tamaa maishani.Anaeleza kuwa vijana hawa huishia kuwa ovyo katika jamii zinazowategemea jambo ambalo huzima matumaini ya baadaye ya jamii hizi.Masuala yaliyoko kwenye kazi hii yalifaa utafiti huu kwani yamejikita kwenye utamaushi kwa vijana unaotokana na hali ya kiuchumi.Utafiti huu uliepuka masuala ya uchumi na badala yake kuegemea tamaa inayokatishwa na masuala ya imani za kidini miongoni mwa vijana huku sababu za utamaushi,athari zake kwa jamii na mapendekezo mwafaka ya hali hii zikiangaziwa.

Matundura(2019)huku akimnukuu mwalimu wake wa chuo kikuu Bw.Crispine Isaboke katika tasnifu yake ya uzamili,anasema kuwa pindi mtu anapozaliwa,moyo wake huwa kana kwamba umetiwa majira mithili ya saa. Kwa mujibu wa Matundura, mtu huwa hajui hatima yake ila inajulikana na Muumba wake pekee.Anadai kuwa linalomtamausha mwanadamu zaidi ni kufahamu kuwa chochote anachoamua kilipangwa pindi tu alipozaliwa na kuwa maamuzi yake yote hudhibitiwa na jaala. Hali hii humnyong’onyeza mwanadamu huyu zaidi na kujiona kiumbe duni aliyetupwa duniani kutaabika katika maisha yake yote.Utafiti wa Matundura ni wa manufaa kwa utafiti huu kwani unajadili kuhusu utamaushi unaosababishwa na ufahamu kuwa maisha hudhibitiwa na jaala na kuwa juhudi za binadamu hazibadilishi lolote.Tofauti ya kazi ya

Matundura na utafiti huu ni kuwa ni kuwa badala ya mtafiti kuengemea jaala,alijikita kwenye kipengele cha dini ili kubaini namna dini inavyotamausha vijana.athari za utamaushi huu kwa jamii ya vijana hawa pamoja na mapendekezo ya kushughulikia utamaushi huu.

Wasike,K(2020) katika tasnifu yake ya uzamili ulioengemea uhakiki wa riwaya ya *Ua la Faraja*, anamwangazia mhusika Omolo aliyetamaushwa na maisha kiasi cha kuishi kwa muda mrefu bila kuoa. Kwa mujibu wa Wasike,Omolo aliishi kwa kujiuliza maswali mengi kuhusu maisha,"Alishangaa kwa nini hata yule mwenye maisha ya shida anapoungua na kukaribia kifo ili hafurahi kuisha kwa shida zake akifa bali huhangaika kujitibu ili apone aendelee na shida zake" (uk23) vile vile mhusika Queen haoni faida ya kuishi na hakuna haja kwa kutia bidii maishani kisha afe. Hili linakazwa na hali yake kuwa alikuwa na ugonjwa wa UKIMWI. Msomi Wasike amezingatia utamaushi wa maisha kwa jumla unaowafanya wahusika wengine kukosa tamaa ya kufanya lolote maishani kwani mwishoni mna kifo. Kazi yenyewe ilikuwa na manufaa kwa utafiti huu kwani ina misingi ya mathara yanayosababishwa na utamaushi. Utafiti huu ulizama ndani ili kufafanua madhara haya kwa upana kwenye kipengele cha utamaushi wa kidini huku kazi yake ikiegemezwa kwa sababu za vijana hawa kutamaushwa na masuala ya kidini,athari zake kwa jamii na kisha mapendekezo ya kukabiliana na hali hii ya utamaushi wa kidini.

Abdallah,M.(2021)katika tasnifu yake ya uzamifu anasema kuwa baada ya vita vya pili vya dunia,maisha yalionekana kutokuwa na maana kwa jinsi vita hivyo vilivyoangamiza mamilioni ya watu. Aidha,maisha yalikuwa magumu kwa kuwa uchumi uliporomoka. Hali hii ya taabu ya kisaikolojia ,ilifanya watu wengi na hasa kutoka magharibi wadai kuwa Mungu amekufa kwa sababu kama angekuwa hai asingewaruhusu kuteseka na kuacha wengi waangamie kama ilivyotokea. Kazi ya Abdallah inaangazia utamaushi uliosababishwa na vita ambao uliathiri watu wa vitengo tofauti barani Ulaya.kazi hii ina manufaa kwa utafiti huu kwani inajadili kwa mapana suala la utamaushi lililosababishwa na vita.Tofauti ya kazi ya Abdallah na ya mtafiti ni kuwa

Mount Kenya University

kinyume na utamaushi uliosababishwa na vita,mtafiti aliangazia utamaushi uliosababishwa na dini kwa kuengemea kipengele cha vijana,athari za utamaushi huu kwa jamii na kisha mapendekezo mwafaka ya kukabiliana na hali hii ya utamaushi.

Adria Fuluge (2022) huku akiangazia riwaya *ya Rosa Mistika* katika jarida lake,anajadili jinsi wahusika mbalimbali wanavyotamaushwa na maisha na kukosa suluhu kwa vitengo vyote ikiwemo dini hadi kufikia maamuzi ya kujiua.Ingawa kwa mkondo  na mchakato mrefu,Rosa anapitia hali nzito ya maisha akitafuta maana ya maisha na anapoona kuwa hakuna suluhu atakalopata anatamauka na kuamua kujitoa uhai.Rosa anafuraia kifo chake kwa sababu kwake huo ndio uhuru aliokuwa anautafuta kama suluhisho la taabu zake.(uk 161). Kazi ya Fuluge ina msingi mwema kwa kazi ya mtafiti kwani inaangazia athari mojawapo ya utamaushi;yaani athari ya kufurahia kifo badala ya uhai.Kwa upande wa kazi ya mtafiti alinuia kushughulikia utamaushi wa kidini miongoni mwa wahusika vijana wa jinsia zote huku akizamia kinachosababisha utamaushi huu,athari zake kwa undani wake na ambazo sio lazima ziwe za kujiua pamoja na njia mwafaka zinazoweza kutumiwa kukabiliana na hali hii nyeti katika jamii karne ya ishirini na moja.

Hivyo kutokana na kazi hizi zote bado kuna mwanya uliojitokeza na ndio maana kwenye utafiti huu, mtafiti alinuia kuuziba kwa kuzingatia suala la sababu za utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana,athari zake kwa vijana hawa na kwa jamii wanamotoka pamoja na mapendekezo ya kukabiliana na utamaushi huu kwa mujibu wa riwaya za *Paradiso* ya John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea* ya Ken Walibora

## 2.2 Misingi ya Nadharia

Wamitila (2003) anaeleza kuwa nadharia ni istilahi inayotumiwa kurejerea kauli au faida za kijumla zinazotegemezwa kwenye uwazaji fulani.Ni mfumo wa mawazo yanayoeleza kuhusu maisha ya mwanadamu na mazingira yake.Utafiti huu uliongozwa na Nadharia ya Udhanaishi

na vile vile Nadhara ya Ubwege.Wataalamu mbalimbali wanajaribu kueleza maana ya udhanaishi kama ifuatavyo;

Kimani Njogu na Rocha Chimera(1999) wanadai kuwa udhanaishi ni nadharia inayoshughulika zaidi na dhana ya maisha ambapo suala kuu ni kuishi ni nini? Wana swali mwanadamu ni wa nini chini ya jua na inahusiana vipi na Muumba wake?Wamilitila,K.W (2003) anadai shida za binadamu zimemfanya ashuku kuwepo kwa Mungu.

Wanjala Simiyu(2012)katika kitabu chake cha fasihi simulizi anasema kuwa udhanaishi ni falsafa au mtazamo wa maisha ulio na kitovu chake katika swala kuwa ,maisha ni nini na yana maana gani kwa binadamu?Ni kwa njia gani mwanadamu anaweza kuyabadilisha maisha yaliyojaa na dhiki,mashaka na huzuni.

Camus (1984)anadai kuwa udhanaishi ni falsafa inayoshughulikia masuala kuhusu maisha ; ni mtazamo unaokagua kwa upembuzi hali ya nafasi ya mtu katika ulimwengu anamoishi.Pia ni falsafa inayozungumzia uhusiano uliomo kati ya mtu na Mungu na iwapo mtu anapaswa kuamini kuwepo kwa Mungu.Nadharia hii ilisaidia kuchunguza vijana wanaoishi katika ulimwengu uliojaa shida na matatizo mengi ambayo yanasababishwa na mwanadamu mwenyewe.Matatizo yanayopitiwa na vijana kama vile ukosefu wa ajira,njaa,vita vya kidini na magonjwa ndiyo yanayowafanya wakate tamaa na kushuku kuwepo kwa Mungu na ahadi zake kwa mwanadamu. Nadharia hii hutumiwa kuhakiki kazi nyingi za fasihi zilizoandikwa na waandishi tofauti na zinazohusu utamaushi wa aina tofauti.

Kimani na Chimera(1999),wanadai udhanaishi unahusiana kwa kiasi kikubwa na mwanthropolojia wa kidenimaki kwa jina Soren Kierkeguard (1813-1855) aliyedai kuwa dini haiwezi kutatua shida zote zinazomkuba binadamu akiwa duniani humu.

Sababu kuu ya kuchangua nadharia hii ni kuwa itasaidia kupambanua dhana kuu ya utamaushi unaokumba vijana na hasa kwa upande wa imani na dini kwa kurejelea riwaya *za Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea.*

### 2.2.1 Mihimili ya Nadharia ya Udhanaishi

Kulingana na Wafula na Kimani (2007) udhanaishi una mihimili ifuatayo;

i) Binadamu hukumbana na taabu halisia katika maisha ya kila siku.

ii) Hupalilia kutokuwepo kwa Mungu na uumbaji wake wa ulimwengu.

iii) Kusisitiza bidii ya binadamu kutaka kufahamu ukweli wa maisha hufikia kikomo kifoni.

iv) Maudhui yaliyo kwenye nadharia hii ni binadamu kuwa huru kivyake ni kuwa na nguvu za kuwaza kufanya maamuzi yake ya moyoni.

v) Taabu na hali ya kuchoshwa na mambo mengi maishani na athari yake.

vi) Kujadili maudhui yenye ukengeushi (hali ya kutamauka na kushuku hali).

vii) Kuchora taswira au picha mbalimbali za maisha ya mateso anayopitia mwanadamu duniani.

viii) Nadharia ya udhanaishi inatilia mkazo kuwa maisha yamejawa na utupu, kihoro, huzuni na hofu hasa kuhusu maisha ya kesho (mbele na nyuma ya binadamu kuna utupu/ombwe/ubatili)

ix) Maisha kujawa na ubwege na kumhakikishia kiumbe huyo kuwa mwisho wa maisha huwa ni kifo.

x) Ni sawa mtu kushiriki katika matendo kama zinaa, ngono za jinsia moja, kuwa na wapenzi wengi na kulewa ili kukidhi mahitaji ya mwili wale.

### 2.2.2 Ubwege

Magare (2002) katika kazi yake ya tasnifu ya uzamili anadai kuwa mwasisi wa nadharia hii ni mwanafililosofia Camus kutoka Ufaransa. Kwa Camus,ubwege huzaliwa baada ya akili kukosa kutosheka na hali ambayo ilikuwa inatarajia.Hali hii hufanya akili labda kufanya maamuzi ya aina mbili; kukubali kukabili hali jinsi ilivyo au kuamua kujitoa uhai.

Kulingana na Camus,binadamu anayeamini kuhusu dini amepotea na vitendo vyake vimejawa na ujinga ,ubwege na havina maana halisi. Lewis (1962:259) anadai kuwa ubwege ni ile hali ya

kukosa utaratibu.Kwa mujibu wa Lewis,mwanadamu hukaa kwenye sayari iliyojaa dhuluma na ameshindwa na kuratibu mipango yake na kuwa anayoyatenda na kutamka hayana uwiano na hali hii ni ya kibwege.

**2.2.3 Sifa za Ubwege**

Kwa mujibu wa Bennett (2011) na Tarantino na Caneso (2009) wanaainisha sifa za ubwege wa Camus kama ifuatavyo:-

i) Ubwege huyasawiri maisha kama yasiyokuwa na maana yoyote.
ii) Wao huona kuwa juhudi za binadamu kujitugia maana ya maisha huwa za kipuuzi
iii) Wanasawiri ubwege ambao unamwonyesha binadamu kama ambaye amekubali kuishi na machungu.
iv) Wao wanamulika juhudi za binadamu za kutafta furaha kama bure na ovyo.
v) Wanawasilisha malalamishi machungu kuhusu binadamu aliyekatishwa tamaa na maisha ya sasa.
vi) Vile vile ubwege husawiri jamii ambayo badala ya kujitolea kidini, imeweza maazimio ya mtu binafsi dhidi ya kila kitu.
vii) Pia ubwege unaonyesha namna silisili zilizounganisha familia na kuyajaza maisha na hisia za maana zilivyokosa athari yoyote kwenye maisha ya sasa.
viii) Pia ubwege husawiri namna wanaojaribu kutimiza malengo yao kibinafsi kupitia kwa mapenzi, maisha yao yanavyosalia bila hisia, na namna wengi wao wanavyong’ang’ana na huzuni na machozi. Hata wale wanaopata mapenzi huwa ni ya muda mfupi na yanayoandamana na mauaji au hisia za udanganyifu.
ix) Kwa mujibu wa Camus(2005) uzee huandamana na aibu ya mwili kimaumbile, kutelekezwa na upweke unawaofanya wengi kufadhaika na kisha kufariki.

Mihimili ya (i),(v),(vii),(viii) na (ix) ya Nadharia ya Udhanaishi inasisitiza taabu halisia anazokubana nazo binadamu katika maisha yake ya kila siku na hivyo kuchoshwa na mambo mengi maishani. Hii ni baada ya kukumbana na ukweli kuwa juhudi zote za binadamu kujaribu

kusaka suluhu ya taabu zake humsukuma karibu na kaburi.Hivyo basi,mihimili hii ilisaidia mtafiti kujadili lengo la kwanza ambalo ni sababu zinazochangia baadhi ya vijana kutamaushwa na dini kwa mujibu wa riwaya ya *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*.Pia, mihimili ya (ii),(iv) na (vi) ya Nadharia ya Udhanaishi inashuku kutokuwepo kwa Mungu na uwezo wake wa uumbaji wa ulimwengu na jinsi binadamu alivyo huru kufanya maamuzi atakayo maishani.Hivyo basi ilisaidia mtafiti kufikia lengo la pili ambalo ni kutathmini athari zinazotokana na utamaushi wa kidini kwa vijana kwa mujibu wa riwaya ya *Paradiso na Kidagaa Kimemwozea.* Kwa upande mwingine Nadharia ya Ubwege ilifaa mtafiti kwani ubwege huzaliwa baada ya akili kukosa kutosheka na hali ambayo ilikuwa inatarajia na hivyo kuteseka.Sifa za (ii),(iv) na (vi) za Nadharia ya Ubwege zinajadili kuhusu juhudi za jamii kukabiliana na hali inayokubana nayo kila uchao.Hivyo basi zilisaidia mtafiti kufikia lengo la tatu la utafiti huu ambalo ni kuchanganua njia mbadala zinazoweza kutumiwa na jamii katika kuondoa utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana katika jamii kwa mujibu wa riwaya ya *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea.*

**2.3 Hitimisho**

Katika sura hii mtafiti ameangazia yaliyoandikwa kuhusu mada ya udhanaishi kwa jumla ambapo ametambua kwamba suala la utamaushi limezangaa kote duniani na linaathiri viwango vyote vya umri. ameona kuwa kuna changamoto za kila aina kwenye nyanja tofauti za maisha zinazofanya watu wa vitengo mbalimbali kukata tamaa maishani. Vile vile ameangazia misingi na sifa za nadharia zilizotumika kwenye utafiti huu pamoja na mihimili yake ambapo ameeleza kuwa mihimili na sifa zake zilimsaidia kuafikia malengo yake ya utafiti.

# SURA YA TATU

# MBINU ZA UTAFITI

## 3.0 Utangulizi

Sura hii imeshughulikia mbinu mbalimbali za utafiti. Aidha maelezo yametolewa kuhusu muundo wa utafiti, wango la utafiti, usampulishaji, eneo la utafiti, mbinu za ukusanyaji wa data, uchanganuzi wa data iliyokusanywa, uwasilishaji wa matokeo na maadili ya utafiti yaliyozingatiwa.

## 3.1 Muundo wa Utafiti

Utafiti huu umechukua muundo wa kimaelezo ambapo ulijikita maktabani. Utafiti umejikita kwenye matini maridhawa za fasihi ya Kiswahili kwa kutumia mbinu tatu kuu; utafiti wa maktaba kwa kiasi kikubwa ambapo usomaji wa vitabu, majarida, magazeti na matini mbalimbali ili kupata ufahamu zaidi kuhusu suala la utafiti huu ulipitiwa, maandishi mengi ya tasnifu za wasomi tofauti yalisomwa., halafu mtandao ulirejelewa kwa nia ya kuweza kuelewa zaidi masuala yanayohusiana na utamaushi wa kidini.

## 3.2 Wango la Utafiti

Uhakiki huu ulilenga athari za udhanaishi wa kidini kwa vijana.  Data katika utafiti huu zilikusanywa kutokana na dondoo zilizokokotwa kwa kurejelea riwaya mbili teule za *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*.

## 3.3 Uteuzi wa Sampuli

Kwa mujibu wa Renatus (2017), sampuli ni sehemu ndogo ambayo mtafiti atavutiwa nayo katika kupata taarifa na kutoa hitimisho la utafiti wake.Sampuli ya kimakusudi ilitumika  kuteua riwaya ya John Habwe *Paradiso(2005)* na ya Ken Walibora *Kidagaa Kimemwozea(2012).*Riwaya hizi mbili zimeandikwa na waandishi tajika wa kazi za fasihi Afrika Mashariki . Riwaya hizi kwa kiasi kikubwa zinaangazia utamaushi wa kidini na maisha kwa jumla unaokatisha matumaini kwa wahusika wengi. Riwaya hizi ziliteuliwa kwa misingi ya namna watunzi wa kazi hizi



Mount Kenya University

walivyoangazia suala nyeti la utamaushi wa kidini kwa upekee wake. Vile vile riwaya hizi mbili zimetungwa katika karne ya ishirini na moja ambapo vijana wengi wamekata tamaa na kukoseshwa matumaini na masuala ya imani na dini kwa sababu ya wanayoyashuhudia kila uchao.

### 3.4 Eneo la Utafiti

Eneo la utafiti huu lilikuwa lile la maktabani kuliko na maandishi mengi ya fasihi andishi hususan utanzu wa riwaya.Data iliyopatikana kule ilisaidia mtafiti kushughulikia athari za udhanaishi wa kidini kwa vijana kwa kurejelea riwaya mbili teule za *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea*.

### 3.5 Ukusanyaji wa Data

Kwa mujibu wa Eugene Taylor( 2021), ukusanyaji wa data ni kitendo halisi cha kutafuta habari muhimu na kuziweka katika kikundi fulani kwa nia ya kumsaidia mtafiti yeyote kuafikia malengo aliyokusudia.Mtafiti alikusanya data yake kwa kusoma kwa kina riwaya ya *Paradiso*(2005) *na Kidagaa Kimemwozea*(2012)huku akidondoa hoja zilizohusiana na utamaushi wa kidini kwa vijana. Vile vile mtafiti alirutubisha data kwa kutalii maktabani ili kusoma vitabu,makala tofauti na tasnifu za wasomi mbalimbali zilizoangazia utamaushi.Pia, mtafiti alipekuapekua mitandaoni ili kujiongezea ufahamu zaidi kuhusu suala lake la utafiti.Ili kukusanya data,vifaa vya utafiti kadhaa vilitumika.Kwa mujibu wa Mulokozi na Mugenda (2003),vifaa ni zile bidhaa ambazo zinahitajika katika kutekeleza kazi yoyote ya utafiti. Kulingana na wataalamu hawa, malengo ya kazi ya utafiti hayawezi kuafikiwa pasipo na vifaa hitajika.Katika utafiti huu,mtafiti alitumia madaftari,kalamu,karatasi za kuandikia,tarakilishi na simu tamba katika mchakato mzima wa kukusanya na kuchambua data yake.Vifaa hivi vilitumiwa ili kurekodi yaliyosomwa kutoka kwa matini yaliyopitiwa.Data iliyopatikana ilihifadhiwa kwenye tarakilishi pamoja na nyingine kwenye simu terezi.

Mount Kenya University

### 3.6 Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Coursera( 2022),uchanganuzi wa data ni mchakato wa kutumia utaratibu murua wa takwimu au umantiki wa data iliyokusanywa ili kufanya maamuzi sahihi. Maamuzi haya yanapaswa kujenga misingi yake kwenye malengo ya utafiti husika.

Data iliyochanganuliwa ilitoka kwa riwaya mbili*; Paradiso(2005)* ya John Habwe na *Kidagaa Kimemwozea(2012)* ya Ken Walibora.Data iliyopatikana ilichanganuliwa kwa kutumia maelezo na tarakimu kwa kuegemea mihimili na sifa za Nadharia za Udhanaishi pamoja na ile ya Ubwege.Mihimili na sifa za nadharia hizi zilisaidia kutambua upekee wa jinsi waandishi wa riwaya hizi walivyoangazia suala nyeti la kukata tamaa na kukosa matumaini katika masuala ya kidini kwa mujibu wa riwaya za waandishi wa riwaya hizo.Mtafiti alijaribu kuratibu kiwango cha asilimia ambacho kila mojawapo wa riwaya hizi inavyoangazia utamaushi wa wahusika mbalimbali. Vile vile maelezo na ufafanuzi zilitumiwa kuwasilisha data ambayo mtafiti aliibuka nayo. Data hii ilisaidia kutathmini viwango ambavyo waandishi wa vitabu hivi walivyofaulu kuangazia suala la utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana.

### 3.7 Maadili ya Utafiti

Kulingana na Mathooko na wenzake (2007), maadili ya utafiti ni uwajibikaji na uelekevu kitabia kuhusiana na haki za wale wote wanaotangamana na mtafiti katika utafiti wake, uwelekevu katika nia na malengo ya utafiti na jinsi ya kutumia matokeo kwa uadilifu ili yaweze kuwa na faida kwa jamii ya binadamu. Barnes (2000) anasema maadili huibuka wakati tunapojaribu kuamua kati ya chanzo cha tendo kwa tendo lingine sio kwa manufaa tu lakini kwa kurejelea mienendo mizuri au mibaya.Kulingana na Massamba (2009), maadili ya utafiti si suala la kidhahania kwani hutokea katika eneo mahususi na kwa watu mahususi. Mtafiti yeyote yule hana budi kutilia maanani vipengele vinavyohusiana na maadili kwenye utafiti ikiwa ni pamoja na kuomba na kukabidhiwa cheti cha kufanya utafiti wa kutunza siri za taarifa, ridhaa ya watafitiwa

Mount Kenya University

na pia hali ya kuchukua picha. Hii ina maana kuwa mtafiti yeyote yule hawezi kuliepuka saula nyeti la maadili.

Katika utafiti huu, mtafiti alipata barua ya kuanzisha utafiti wake kutoka chuo kikuu cha Mount Kenya. Pia mtafiti aliomba kibali kutoka  kwa kitengo cha idhini za ukusanyaji wa data nchini NACOSTI.Utafiti huu ulifanywa kwa uwazi na uadilifu mkubwa huku nyadhifa zote husika zikiheshimiwa.

### 3.8 Hitimisho

Katika sura hii,mtafiti ameangazia mbinu zilizotumika kukusanya data, uteuzi wa sampuli na ukusanyaji wa data. Vile vile,vifaa vilivyotumika katika mchakato mzima wa ukusanyaji wa data,jinsi data ilivyochanganuliwa na pia maadili yaliyoongoza mchakato mzima wa utafiti huu yameangaziwa.

Mount Kenya University

## SURA YA NNE

## UCHANGANUZI WA DATA NA UFASIRI WA MATOKEO YA UTAFITI

### 4.0 Utangulizi

Katika Sura hii tumeangazia historia ya waandishi John Habwe na Ken Walibora kwa misingi ya maisha yao ya awali pamoja,tajriba zao aidha na kazi zao mbalimbali. Kwenye sura hii pia uchanganuzi na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti yametolewa kwa kuegemea malengo ya utafiti.Vile vile,sura hii tumeshughulikia mbinu mbalimbali zilizopendekezwa na waandishi John Habwe na Ken Walibora kukabiliana na udhanaishi wa kidini kwa vijana.Data iliyokusanywa imewasilishwa kwa maelezo ya kinadhari kama ilivyopendekezwa kwenye sura ya tatu.

### 4.1 Historia fupi ya John Habwe

John Hamu Habwe alizaliwa mnamo Disemba 12,1962 maeneo ya Luanda Kaunti ya Vihiga Magharibi mwa Kenya. Alijiunga na shule ya msingi ya Ebukhaya ambapo alihitimu mtihani wa kitaifa wa darasa saba(CPE) mwaka wa 1976. Habwe alijiunga na Shule ya Upili ya Ebwali na kuhitimu mwaka wa 1980 alipokamilisha kidato cha nne. Baadaye alijiunga na Shule ya Upili ya Kapkatet katika kaunti ya Kericho na kuhitimu kidato cha sita mwaka wa 1982. Alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi na kumaliza shahada ya kwanza ya elimu (B.A.) mnamo mwaka wa 1987. Kisha alijiunga na chuo hicho hicho na kufanya shahada Uzamili ambapo alihitimu mwaka wa 1989. Kiu ya elimu ilimsukuma Habwe kuzamia masomo yake na kuhitimu na shahada ya Uzamifu vile vile kutoka chuo kikuu cha Nairobi mwaka wa 1999. John Habwe ambaye kwa muda mrefu amekuwa mhadhiri katika Chuo Kikuu cha Nairobi,amewahi kuwa mwalimu katika Shule ya Upili ya Busiratsi, Bunyore mwaka wa 1983 ambapo alihudumu kama mwalimu mkuu wa shule hiyo.Pia,Habwe alitoa huduma zake kama mhadhiri wa muda (*Part Time Lecturer*) katika Chuo kikuu cha Maseno (2003-2004),Mtahini wa Nje (*External Examiner*) katika Chuo

Kikuu cha Moi (2010-2016). Zaidi ya hayo,Habwe amewahi kupata matuzo mbali mbali kwa ugwiji wake wa uandishi wake. Baadhi ya matuzo hayo ni kama vile; *Wahome Mutahi Literary Prize Award in Kiswahili* ya Riwaya ya *Paradiso* mwaka wa 2006,*Wahome Mutahi Literary Prize in the Kiswahili Category* ya Riwaya ya *Cheche za Moto* mwaka wa 2010,*Jomo Kenyatta Textbook Centre Kiswahili Literary Award* ya Riwaya ya *Pendo la Karaha* mwaka wa 2015 na *Wahome Mutahi Award for Literature* ya Riwaya ya *Kovu Moyoni* mwaka wa 2016. Pamoja na riwaya ya *Paradiso* Habwe ameandika riwaya nyingine za kusisimua ulimwengu wa fasihi kama vile*;Maumbile si Huja (1995),Maisha Kitendawili (2000),Fumbo la Maisha (2009),Safari ya Lamu* (*2011),Pamba (2011) na Hidaya Yangu (2018)* miongoni mwa riwaya nyingine. Kwa sasa John Habwe ni Profesa Mwandamizi katika Chuo Kikuu cha Nairobi ambapo amekuwa mhadhiri kwa miongo mitatu.

**4.2 Historia fupi ya Ken Walibora**

Ken Walibora ambaye jina lake halisi ni Kennedy Waliaula alizaliwa tarehe 6 Januari,1965 katika kijiji cha Baraki Kaunti ya Bungoma Ukanda wa Magharibi mwa Kenya. Ken alianza elimu yake ya msingi katika shule ya St. Joseph’s Kitale mwaka wa 1971.Baada ya kufanya mtihani wa kitaifa mwaka wa 1978,Ken alijiunga na Shule ya Upili ya Olkejuado katika Jimbo la Kajiado na kuhitimu kidato cha nne mwaka wa 1982. Baadaye alijiunga na Shule ya Upili ya Koelel,Gilgil viungani mwa Kaunti ya Nakuru alipokamilisha kidato cha sita mwaka wa 1984. Waliula alikuwa mwalimu wa lugha za Kiswahili na Kiingereza katika Shule ya Upili ya Sitatunga katika Wilaya ya Trans Nzoia miaka ya 1985 na 1986. Baadaye alijiunga na Taasisi ya Utawala ya Kenya(*Kenya Institute of Administration*) na kupata mafunzo ya huduma za jamii hadi mwaka wa 1988. Kati ya mwaka wa 1988 na 1996,Ken aliajiriwa na kufanya kazi katika Wizara ya Mambo ya Ndani na Turathi za Kitaifa. Ken alijiunga na Shirika la Utangazaji la KBC mwaka wa 1996 kwa ugwiji wake wa lugha ya kiswahili na kuwa mtangazaji na mhariri wa habari. Mwaka wa 1999,Ken alijiunga na Kampuni ya Usambazaji wa Habari ya *Nation Media Group* ambapo alitoa huduma zake hadi mwaka wa 2004 alipopata ufadhili wa masomo na

Mount Kenya University

kwenda Marekani kusomea shahada za Uzamili na Uzamifu katika Chuo Kikuu cha Ohio State,Columbus. Hii ilitokea kwa vile bado akiwa mfanyikazi katika Kampuni ya *Media Group*, Ken alijiunga na Chuo Kikuu cha Nairobi alikosomea Fasihi ya Kiswahili na kuhitimu kwa kiwango cha juu zaidi (*1st Class Honours*) mnamo Mei 2004.

Ken aliwahi kuwa mhudumu katika Chama cha Kiswahili cha Taifa Kenya (CHAKITA) na katika Akademia ya Afrika ya Lugha (ACALAN) iliyo na makao yake katika jiji la Bamako,Mali. Ken alikuwa mwanzilishi wa Chama cha Wanahabari wa Kiswahili cha Afrika Mashariki(CHAWAKIMA) na pia mwanachama wa Chama cha Kiswahili cha Afrika Mashariki(CHAKAMA). Ken aliwahi kutuzwa kama mtangazaji bora wa Kiswahili na Shirika la Wanahabari la Kenya mnamo mwaka wa 2003 na pia aliwahi kuteuliwa kama mtangazaji bora wa Kiswahili wa runinga kwa miaka mitatu mfululizo;2002,2003 na 2004. Licha ya kuandika riwaya iliyosisimua ulimwengu wa fasihi ya *Kidagaa Kimemwozea*,Ken ameandika vitabu vingine kama vile;*Siku Njema*(*1996*),*Ndoto ya Amerika*(*2001*),*Kufa Kuzikana* (*2003*),*Ndoto ya Almasi* (*2006*),*Nasikia Sauti ya Mama*(*2014*) miongoni mwa vitabu vingine tajika. Maisha yenye tunu na tamasha ya Ken Walibora yalifikia kikomo chake mnamo Aprili 10,2020 alipogongwa na gari katika Barabara ya Landhies,kwenye Mtaa wa Muthurwa jijini Nairobi.

### 4.3 Muhtasari wa Riwaya ya *Paradiso*

Riwaya ya *Paradiso* iliandikwa na John Habwe na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2005. Kulingana na TUKI 2013:451,neno '*paradiso'* lina maana ya edeni,pepo au firdausi. Kulingana na TUKI 2013:458,neno '*pepo'* lina maana ya mahali patukufu panapoaminiwa kuwa baada ya kufufuliwa na kulipwa matendo yao mazuri walioishi kulingana na amri za Mungu wataishi milele. Ingawa *Paradiso* ni riwaya yenye mkusanyiko mwingi wa maudhui,maudhui makuu kwenye riwaya hii ni yale ya Unafiki wa kidini unaoendelezwa na viongozi wa dini pamoja na waumini wake katika matukio mbalimbali yanayopatikana kwenye riwaya hii. Unafiki huu wa kidini unaotokea unaendelezwa na wahusika tofauti na kudhihirika kwa matendo kama vile ya;ufisadi,mipango ya kando,vita baina ya waumini,chuki,anasa,biashara kwa jina la

Mungu na kujitajirisha kwa kutumia Neno la Mungu miongoni mwa vitendo vingine. Matendo haya ni kinyume na mafundisho ya dini. Hata hivyo neno '*paradiso'* ambalo ndilo anwani iliyopo kwenye jalada la riwaya hii lina maana tofauti kama inavyodokezwa na mwandishi pamoja na wahusika mbalimbali kwenye kitabu hiki. Maana za neno hili ni kama ifuatavyo;

i)Wendawazimu na kuwa kwenye ulimwengu tofauti na watu wengine kama ilivyo kwa mhusika Musa (uk 75)

ii)Kuishi katika paradiso yenye magari mengi jinsi anavyodai mhusika Musa (uk66)

iii)Kuwa na magari mengi na kula sadaka na zaka za kanisa wanavyofanya wahusika Joshua na mkewe Lona uk (48;67;68;)

iv)Kuwa na wake wengi na kujihusisha na ukahaba kama anavyodai mhusika Mango akiwarejelea wahusika Sakina na Zuhra (uk 10)

v)Mahali pazuri pasipo na magonjwa,umaskini,kuchoka wala haja yoyote kama anavyodai Mhubiri Michael (uk 95.)

Kulingana na maelezo ya maana ya neno 'paradiso',ni dhahiri kuwa maana yake ya ujumla ni ulimwengu ulio tofauti na ule wa kawaida. Mwandishi na wahusika kwenye riwaya hii wanawakilisha jamii pana ya mwanadamu wa kawaida tu ilhali mazingira ambayo vitushi vinatokea yanasawiri mazingira halisia anamoishi mwanadamu.

Riwaya hii ya *Paradiso* imengawanyika katika sura kumi na nane zilizomo kwenye kurasa 230 ambazo kila sura ina mvuto wake unaomfanya msomaji kuwa na ari ya kubukua kitabu chenyewe kujifahamisha zaidi kuhusu maudhui makuu ya unafiki wa kidini. Ingawa dini hudhaniwa na jamii kama chombo cha usalama na afueni kwa ulimwengu uliovurugika,yanayojitokeza katika riwaya hii ni tofauti kabisa kwani baadhi ya viongozi wa dini na washirika wao wanatenda kinyume na matarajio na mafundisho ya dini. Maadili ya baadhi ya waumini yameoza kiasi cha

kuwafanya vijana wanaozidi kuziduka kila uchao kukosa kuona maana ya kujihusisha na dini. Hata hivyo,riwaya hii ya *Paradiso* inadodoa maudhui mengine kama vile,ndoa,ukware,nafasi ya kanisa kwenye jamii,ufisadi,tamaa, elimu,migogoro,umaskini na utabaka miongoni mwa maudhui mengine. Riwaya hii inaweza kuainishwa kama ya uhalisia kwani masuala yanayojadiliwa ndani ya kitabu yanalingana na yale yanayoshuhudiwa kwenye ulimwengu wa kawaida tu. Maabadi zinawakilishwa na makanisa ya *Bethany* na lile la *New Jerusalemu* ilhali viongozi wakuu wa dini wanawakilishwa na Askofu Joshua na mkewe Kasisi Lona pamoja na Mhubiri Michael.

### 4.4 Muhtasari wa Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*

Riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea* iliandikwa na Ken Walibora na kuchapishwa kwa mara ya kwanza mwaka wa 2012. Riwaya hii imegawanyika katika sura 10 zilizo kwenye kurasa 162. Ingawa riwaya hii ina masuala chungu nzima yanayojadiliwa na mwandishi,suala kuu lililopo kwenye kitabu hiki ni namna ndoto walizokuwa nazo Waafrika walipokuwa wakipigania uhuru zilipogeuka na kuwa jinamizi isiyotarajiwa.Afrika inawakilishwa na taifa la Tomoko na eneo dogo la Sokomoko linaloongozwa na Mtemi Nasaba Bora.Wazalendo na wanyonge waliokuwa mstari wa mbele kupigania uhuru na kumfukuza mkoloni mweupe waligeukwa na viongozi wa kiafrika pindi tu uhuru ulipopatikana. Neno ‘Kidagaa Kimemwozea’ ni istilahi iliyotumika kuonyesha namna matarajio ya Waafrika yalivyotingwa na uongozi wa Waafrika wenzao kwa kukosa kutimiza ahadi zao na kutamausha nyoyo zilizokuwa na matarajio makuu baada ya uhuru. Kulikuwa na wanyonge waliowakilishwa na wahusika kama vile Imani,Amani,Matuko Weye,Uhuru na DJ miongoni mwa wengine ambao nyoyo zao zilitamauka kiasi cha kupatwa na msongo wa mawazo ulioathiri na kuvuruga akili zao. Familia za waliopigania uhuru kama vile Mwinyihatibu Mtembezi hazikuwa na chochote cha kujivunia ila kutaabikia kwenye nchi yao huru. Maudhui makuu kwenye riwaya hii ni yale ya Usaliti ambapo raia wanasalitiwa na viongozi wao kwa kupitishwa dhuluma za kila aina na hata wengine kuuawa pasipo na hatia. Raslimali zinazopaswa kuauni wananchi zinawakilishwa na maji ya Mto Kiberege ambapo

badala ya maji haya kuleta uhai yanakisiwa kuwa ni maji ya mauti. Hadithi ya kitabu hiki inasawiriwa kupitia safari ya wahusika wawili Amani na Imani ambao wanaanza safari kutoka makwao kuelekea eneo la Sokomoko kusaka kazi ambazo labda zingeleta afueni kwa maisha yao. Wahusika hawa wanavunja mwiko kwa kunywa maji ya Mto Kiberege yaliyodhaniwa na wenyeji kuwa maji ya mauti. Kitendo cha kutoathiriwa na maji yale kinabadili dhana ya wakaaji wa Sokomoko na kuweka peupe kuwa hata haramu inaweza kuwa halali na halali kuwa haramu. Wanapofika katika kijiji cha Sokomoko, Amani na Imani wanaajiriwa na ndugu wawili;Mtemi Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu mtawalia. Ingawa  waajiri hawa walikuwa dhalimu kwa Amani na Imani, vijana hawa wanafanya bidii za mchwa kwa kazi zao kwani nia yao ilikuwa kufanya upelelezi ili kugundua waliopoka mali ya familia zao.

Inadhihirika kuwa jasho la wasomi hufaidi wengine kwani Mwalimu Majisifu ni mwizi wa miswada ya wasomi ambapo badala ya kuchapisha kazi za wasomi hawa,anawajulisha kuwa kazi zao ni chapwa na kisha kuzichapisha kwa jina lake na kuziuza. Hata hivyo,Amani na Imani wanaongoza umati wa watu na kuwazidua kuhusu haki zao walizonyimwa na viongozi wao. Kupitia kwao inadhihirika kuwa Mtemi Nasaba Bora ambaye anawakilisha viongozi wa Afrika baada ya uhuru ni mnyakuzi mkuu wa ardhi za wanyonge. Inadhihirika kuwa viongozi hubadili vyeti vya kumiliki ardhi na kuwapa wenyeji vyeti bandia kwa minajili ya kunyakua ardhi zao. Baada ya siri za Mtemi Nasaba Bora kuwekwa wazi anajiona ombwe tupu na asiyeweza kuishi kwa aibu miongoni mwa watu wake na kwa hivyo anaamua kujitoa uhai kwa kujitia kitanzi. Amani anayewakilisha wanamapinduzi anaongoza utawazaji wa mtemi mpya na kuahidi kuwa makosa yaliyotokea awali hayatarudiwa.

Pia anawazidua raia kuwa macho kukabiliana na dhuluma yoyote ile ambayo ingezuka na kuendelezwa na kiongozi mwingine. Mabadiliko yanayoletwa Sokomoko na Amani na Imani yanadhirisha kuwa hakuna jambo lisilowezekana Barani Afrika.Wanyonge wakiungana pamoja wanaweza kuleta mageuzi makubwa na kubadilisha hali ya kiuchumi ya jamii zao.Riwaya hii

pia ina maudhui mengine kama vile;ufisadi,unafiki wa kidini,dhuluma,ulevi,wizi na ukware miongoni mwa maudhui mengine.

### 4.5 Uwasilishaji wa Matokeo ya Utafiti

Yafuatayo ni maelezo kuhusu uchanganuzi wa data mbalimbali iliyokusanywa kwa mujibu wa malengo ya utafiti.

#### 4.5.1 Sababu za Kidini Zinazowatamausha Vijana katika Paradiso na Kidagaa Kimemwozea.

#### 4.5.2 Mipango ya Kando baina ya Waumini.

Mpango wa kando ni hali ya kuwa na mpenzi wa kingono nje ya ndoa. Pia huitwa jicho la nje. Kila dini yenye waumini huwa na sheria zake kuhusu ndoa ambapo uaminifu hudhaminiwa na iwapo mwanandoa mmoja amefanya mapenzi nje ya ndoa basi huwa amevunja sheria za dini yake kuhusu suala hili la uaminifu.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia mipango ya kando miongoni mwa wanadini. Michael ambaye alikuwa mchungaji katika kanisa la *Bethany Bible Church* mtaani Kibera ana uhusiano wa kimapenzi na Patricia licha ya kuwa na mke wake wa halali Lydia. Kama inavyodhihirika katika dondoo ifuatayo;

‘’*Michael alijikuta mwili umemzidi na kumkumbatia Patricia hapo tu Patricia alipokuwa akilia. Katika mkumbatio huo, Michael alishtukia amempiga kisi Patricia. Patricia naye akajibu kwa kushikilia ulimi wake humo kinywani. (uk 152).*

Uhusiano wa mapenzi kati ya Michael na Patricia ulitoa matokeo ya kuzaliwa kwa mtoto. Vitendo vya mchungaji Michael vinamfanya kijana huyu wa kike Patricia kutoshswa na masuala ya dini. Vile vile, licha ya Lona kuwa mke wa Askofu Joshua alikuwa na mwanamume mwingine wa pembeni. Haya yanadhihirika kwenye dondoo lifuatalo;

‘*Lona alikuwa pale pale, kulikuwa na mume wa zaidi. Lona hakujua amfuate Joshua au yule mume mwingine. Lona alielea kati ya wanaume hao wawili’. (Uk 136)*

Kijana Patricia anawakilisha baadhi ya vijana wanaotamaushwa na dini katika jamii ya karne ya ishirini na moja wanapogundua kuwa hata wahubiri wanaopaswa kuwa kielelezo cha wanachokiamini katika jamii wanafanya mapenzi nje ya ndoa.

Ken walibora katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea(2012),*anamwangazia Mtemi Nasaba Bora mtoto wa kasisi na kiongozi wa Tomoko aliye na jicho la nje licha ya kuwa na mke wake Bi. Zuhura. Mtemi Nasaba Bora licha ya kuwa mtoto wa kasisi, ana mpango wa kando na Lowela bintiye Bw. Maozi kinyume na matarajio ya jamii inayoakisi watoto wa viongozi wa dini kuwa waadilifu. Mapenzi yao yananata hadi anafika nyumbani kwake alfajiri na kudai kuwa ametoka kusuluhisha migogoro ya mashamba. Mwishowe Mtemi, mtoto wa kasisi anampachika Lowela mimba na kumficha kwenye shamba moja lake kule Baraka. Haya yanadhihirika kwenye barua iliyoandikiwa Mashaka na Ben Bella dadake Lowela kwenye nukuu ifuatayo;

‘‘*Nilipofika kwetu nyumbani kutoka jela nilikuta wazazi wangu wakitapatapa kumtafuta dadangu Lowela…Hatukujua yuko wapi. Katika pandashuka na pitapita zangu nikamkuta kule Baraka kwa shamba lingine la babako.*’’ (uk 81)

Kitoto kilipozaliwa Mtemi Nasaba Bora mtoto wa kasisi anakiweka mlangoni mwa kibanda cha Amani na kupangaza kijana huyu malezi asiyoyaamkia wala kuyalalia. Inabidi Imani kuacha kazi kwa Mwalimu Majisifu ili kusaidia Amani katoa malezi. Vijana Lowela, Amani na Imani wanakosa kuona faida yoyote ya kujihusisha na masuala ya dini kwani wanaoitanishwa na dini wana vituko vya kiajabu tu badala ya kuwa kielelezo kwa wasio na mwao nayo. Utamaushi wa kidini miongoni mwa vijana hawa ni kiwakilishi tosha kwa vijana wa karne ya 21 wanaotoshwa na dini baada ya kutambua kuwa hata viongozi wa dini na baadhi ya watoto wa makasisi wanaotarajiwa kuwa waadilifu wana mipango ya kando hata na wasichana wa kike ambao hawajaolewa. Jamii inatarajia watoto wa watumishi wa Mungu kuwa waadilifu lakini kitendo cha Mtemi Nasaba Bora aliye mtoto wa kasisi kinakwenda kinyume na matarajio haya.

### 4.5.3 Mifarakano ya Madhehebu

Mafarakano ni hali ya kutoelewana baina ya watu au makundi kwa kubishania kitu fulani. Kutoelewana huku hutokea baada ya mtu au kikundi Fulani kukosa kuridhika na hali fulani. Kulingana na *Mohamed* (2013), mafarakano hutokea baada ya watu fulani kunyimwa nafasi ya kumiliki vyeo au viti fulani katika uongozi. Baada ya Uprotestanti kuzaliwa mnamo karne ya 15, madhehebu tofauti yamekuwa na mafarakano ya mara kwa mara hasa kuhusu uongozi na matumizi ya zaka na sadaka maabadani. Hali hii imezua uzao wa maelfu ya madhehebu duniani kote. Hali hii inawafanya vijana hawa kuzidi kushuku kuwepo kwa Mungu kila uchao wanapozidi kushuhudia mafarakano ya dini zilizokuwa na umoja hapo awali. Kwa vijana hawa, dini ni chombo kilichoanzishwa na binadamu kwa lengo la kudhulumu binadamu mwenzake anapojaribu kujinufaisha.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso*, anaangazia mfarakani maabadani aporejelea mivutano iliyotokea katika kanisa la *New Jerusalem* kama ilivyo kwenye dondoo hapa chini;

'…*Kanisa la New Jerusalemu lilingawanyika katika makundi mawili hatimaye. Kundi moja lilimwunga mkono Joshua na jingine likamuunga mkono Michael. Kila Jumapili vidoko, uvumi., udhabinadhabina vilitawala. Huyu alisema huyu kwa hili na yule mwingine akamsema mwenzake. Suala la Mungu na paradiso ya baadaye halikuwa kiini tena. Kundi la Michael lilisisitiza kuna uhuru wa kukaa hali kundi la Joshua lilitaka liondoke.'(uk77)*

Matokeo ya mifarakano hii ilidhihirika wazi kwani baadhi ya vijana walihamia makanisa mengine na wengine kuacha kuhudhuria ibada. Hali hii sio tofauti na ile inayoshuhudiwa katika maabadi mengi katika jamii ya karne ya 21 hali ambayo inafanya vijana na haswa waliosoma kuacha kujihusisha na masuala ya dini na kujipa shughuli zao siku zilizotengwa kwa ibada hizi.

Ken Walibora katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea* anaangazia mifarakano ya maabadani kwenye mazungumzo ya Mwalimu Majisifu na kaka yake mkubwa Mtemi Nasaba Bora walio watoto wa kasisi nyumbani kwake katika nukuu ifuatayo ;

"*Kumbuka marehemu baba yetu alikuwa kasisi ndugu yangu. Alikuwa akisema kwamba walevi hawataingia katika ufalme wa mbinguni"…"Hizi kurani zako ndizo zinifanyazo nisije huku ndugu yangu." (uk 93)*

Maneno ya Mwalimu Majisifu yanadhihirisha jinsi viongozi wa kidini wanavyoshindwa na kutatua migogoro yao kiasi cha kufanya waumini wapigane na walio na imani hafifu katika jamii ya leo na haswa vijana waliopevuka kutupilia mbali imani zao kwa masuala ya dini.

### 4.5.4 Ulaji na Matumizi Mabaya ya Zaka, Sadaka na Matoleo

Zaka ni toleo la sehemu ya mapato ambalo muumini wa dini fulani anapaswa kutoa. Ni kiwango maalumu cha mali kinachotolewa wakati maalumu kwa watu maalumu. Sadaka ni toleo la chochote kama vile chakula, vitu au wanyama kwa lengo la juu hasa la kidini ili kumheshimu Mungu na kujiombea fadhili fulani kutoka kwake. Kulingana na kitabu kitakatifu cha Wakristo Biblia, ilikuwa ni lazima zaka na sadaka zitolewe kulingana na torati za Mtume Musa. Vitabu vitakatifu vinavyoenziwa na waumini vimetoa utaratibu wa matumizi ya matoleo ya maabadani. Iwapo kutakuwa na matoleo yoyote maabadani basi yanapaswa kusaidia walio taabani bali sio kutumiwa kutajirisha viongozi wa kidini. Ulaji na matumizi mabaya ya zaka na sadaka unazidi kufisha vijana wengi moyo kwani kulingana nao viongozi wa kidini wanazidi kujitajirisha huku waumini wakizidi kumasikinika kila uchao.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia matumizi mabaya ya zaka na sadaka pale ambapo Omae, kiongozi wa huduma ya vijana pale *New Jerusalem* anawaambia waumini kuwa matoleo yamepungua. Omae anawaudhi waumini anaposema kuwa Jumapili iliyofuata vifuko vya sadaka vingekuwa mbele na kila mmoja angetakiwa kupeleka zaka zake akionekana na kila mtu kwani kunao walioudhuria ibada bila yao kutoa chochote. Tangazo hili la Omae liliudhi washirika na wakaanza minong'ono ya chini kwa chini. Mzee mmoja ndiye alipasua barika bila woga inavyodhihirika hapa chini ;

"*Ametuchosha huyu bwana na habari za zaka. Kila siku zaka. Asiyejua habari za zaka nani* ? *Hajui kuna watu wengine hawana pa kutoa hizo zaka. Hata kula hawawezi kula. Tena hizo pesa si wanazila wao.'' (uk 54)*

Maneno ya mzee huyu ni dhihirisho kuwa badala ya zaka na sadaka kusaidia wasiojiweza, zinaliwa na viongozi wa kidini. Hii ndio sababu wanalazimu kila mmoja atoe huku akionekana

asije akahepa utoaji. Hali hii ya ulaji wa matoleo inawaudhi Omae na vijana wenzake na kufifisha imani yao kwenye dini baada ya kugudua kuwa wanafaidisha wachache. Mtazamo wa Omae na vijana wenzake ni kioo angavu cha jinsi vijana katika jamii ya leo wanaoshibishwa na dini kila uchao wanapogudua kuwa badala ya matoleo kuwasaidia walio na mahitaji katika jamii yamekuwa kitenga uchumi kwa viongozi wachache wa kidini.

### 4.5.5 Maabadi kuwa Mali ya Familia

Familia ni kikundi cha watu wanaokaa pamoja kama baba, mama na watoto. Kikundi hicho mara nyingi ni sehemu ya kundi kubwa zaidi la ukoo unaounganisha watu wenye asili katika uzazi wa pamoja. Maabadi ni mahali popote pa kufanyia ibada kama vile hekalu, kanisa, msikiti au mahali popote patakatifu kulingana na wahusika fulani. Pia ni eneo maalumu lililojengwa ambalo mtu au kundi la watu hukutana kufanya ibada au kujifunza masomo ya kidini. Maana hii ni kiini tosha kuwa maabadini panapaswa kuwa mali ya watu wengi kutoka jamii tofauti na sio kutoka familia moja. Hata hivyo, miaka ya hivi karibuni kumetokea kasumba ambayo familia fulani zimekuwa zikimiliki maabadi kama mali yao. Familia fulani zimekuwa zikitumia washirika kama kitenga uchumi ili kujitajirisha tu bila kujali waumini wanaoitanishwa na ushirika huo. Hali hii imevunja waumini vijana wa karne ya 21 moyo na kuamua kuandama mikondo yao ya maisha.

Ken Walibora katika riwaya yake *Kidagaa Kimemwozea* anamzungumzia baba yao Mtemi Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu ambaye alikuwa kasisi. Badala ya kuwakuza wengine kutoka jamii zingine wawe makasisi, mzee huyu alimsaidia mwanawe Mwalimu Majisifu kwenda ng’ambo kusomea ukasisi ili achukue mkondo wa ukasisi wa baba yake na kuiweka boma ya mzee huyu kwenye kilele cha uongozi wa kidini. Haya yanadhihirika kwenye dondoo iliyo hapa chini;

‘‘*Majisifu alikuwa kaelimishwa na misheni kama nduguye mkubwa*. *Ingalikuwa kwake vigumu kwenda ngambo alikoenda lau kama si* pandashuka *za babake kasisi.Alitarajiwa kusomea ukasisi ili aandame nyayo za babake.’’ (Uk 27)*

Kauli hii ni dhihirisho tosha kuwa ingawa kasisi huyu alikuwa mtumishi wa Mungu alipendea mtoto wake asomeshwe na misheni ili awe kasisi kama baba yake na kuendekeza utumishi wa Mungu kwenye familia hii. Hali kama hii inavunja moyo kwa vijana wanaotarajia kuelimika kidini kwani wanaona udini unaandamana kulingana na jinsi watu wanavyojuana kifamilia.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia maabadi kama mali ya familia pale ambapo anasema kuwa Joshua alibakia kuwa Askofu pale *New Jerusalem* huku mkewe Lona akichukua mahali pa Michael kama kasisi naye mtoto wa mjomba wake Nyamongo akichukua nafasi ya Musa kama mhubiri.

'' *Lona sasa ndiye aliyepachukua mahali pa Michael. Alikuwa mmojawapo katika makasisi wa New Jerusalem mbali na Nyamongo aliyepachikwa mahali pa Musa. Nyamongo alikuwa mhubiri…sasa Lona alipopewa cheo hicho cha ukasisi Joshua aliona kakamilika''* (uk 79).

Hii ni ishara tosha kuwa kanisa la *New Jerusalemu* lilikuwa mali ya familia moja huku vijana waliopevuka wakinyimwa nafasi ya uongozi. Uongozi uliopo kwenye kanisa hili la *New Jerusalemu* hauna tofauti kubwa na jinsi hali ilivyo kwenye maabadi mengi ya jamii ya leo hali inayozidi kuvunja mioyo ya vijana waliosoma na kupevuka katika jamii ya karne ya ishirini na moja.

### 4.5.6 Biashara kwa Jina la Mungu.

Biashara ni kitendo cha kubadilishana bidhaa kwa bidhaa au bidhaa kwa pesa labda. Biashara nyingi hufanyika kwa kushtukia au mahali palipotengwa na siku maalumu zilizotengwa. Hata hivyo ni kinyume cha maadili kwa biashara kufanyiwa mahali patakatifu au maabadani kwa mujibu wa imani za waumini.

John Habwe kwenye riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia biashara maabadani anapodai kuwa baada ya polisi kudokezewa kuwa kwenye kanisa la *New Jerusalem* kulikuwa na biashara haramu ya mihadarati na madini ilibidi waende kule kufanya uchunguzi wao kikamilifu ili kuhakikisha ukweli wa madai hayo. Polisi walipofika pale kanisani, Judy mke wake Boribori

Mount Kenya University

alidinda kuwafungulia na ikabidi wavunje mlango kuingia ndani. Walipoingia pale ndani, waliyoyaona yaliwaatua nyoyo. Haya yanadhihirika kwenye dondoo iliyo hapa chini ;

‘’*Polisi walipata mihadarati ya aina ya hashishi, heroine, bangi na mihadarati mingine. Jibwa lao liliwasaidia kunusa sehemu mbalimbali za chumba kilicho na mwanga hafifu. Hawakupata mihadarati tu bali walipata zebaki, almasi na dhahabu.’’ (Uk 198).*

Vile vile mwandishi John Habwe anarejelea kashfa ya miezi minane iliyotangulia ambapo makanisa yalikuwa na kashfa ya ulawiti na kuuza wasichana wadogo kama watumwa wa mapenzi katika nchi za ng’ambo kwa kuwahadaa wanawatafutia kazi (uk 207). Hali hii ya biashara inawavunja nyoyo watoto na vijana wanaojawa na hofu ya kujihusisha na dini. Vituko hasi vya biashara haramu kwenye kanisa la *New Jerusalemu* si geni katika jamii ya leo. Misikitini, mahekaluni, makanisani miongoni mwa maabadi mengine yaliyotapakaa kwenye dunia nzima yamekuwa yakigonga vichwa vya habari kwa kuripoti biashara haramu kwa jina la Mungu. Hali hii inazidi kuwatia vijana wa jamii ya leo hofu kwenye masuala ya dini kwani wanahofia kufanywa kitenga uchumi na kulawitiwa kwenye maabadi jinsi inavyorejelewa na mwandishi John Habwe.

### 4.5.7 Ufisadi Miongoni mwa Viongozi wa Dini.

Ufisadi ni hali ya mtu kupata kisicho chake kwa njia isiyofaa. Pia ni ile hali ya kutoa hongo kwa mtu mwingine kwa nia ya kutaka kupendelewa kwa namna Fulani. Kulingana na ripoti ya Shirika la Umoja wa Kimataifa duniani (UN) 2022, ufisadi ni mojawapo wa masuala yanayotishia kuwepo kwa amani na ulizi duniani. Ufisadi umefifisha maendeleo duniani kwani rasilimali zinazotengewa miradi tofauti ya kimaendeleo zinaishia mifukoni ya watu binafsi. Kutia msumari moto kwenye kidonda ni kuwa ufisadi unaendelezwa na viongozi wa kidini wanaotarajiwa kuwa mwanga katika jamii inayozidi kuoza kila uchao. Sio ajabu kupata kuwa kesi nyingi za ufisadi zinawahusu viongozi wa madhehebu tajika duniani wanaotapeli waumini wao kwa kutumia vitabu vitakatifu na jina la Mungu.

John Habwe kwenye riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia ufisadi anaporejelea mhusika na mchungaji Boribori akijaribu kuhonga jaji Moriasi ili umwonee huruma kwenye kesi inayomkabili ya biashara ya mihadarati na madini kwenye kanisa lake la *New Jerusalem*. Hali hii ya ufisadi inadhihirika kwenye dondoo hii ;

''*Ningependa unisaidie…Ningependa nisaidiwe katika kesi hii inayonikabili…Mimi naomba unijaribie tu. Mungu atafungua njia ninajua… Moriasi na Boribori walirudi kutoka sehemu ya chemba. Boribori alidondoka silingi milioni moja. Aliitoa kama chai kwa jaji Moriasi (uk 212)*

Ingawa Boribori alitaka kuonewa huruma na jaji, mambo yalienda kinyume na matarajio yake kwani jaji aliwatuma jela kwa kuwapata na hatia ya kufanya biashara haramu ya mihadarati na madini. Wanaacha kanisa mikononi mwa waumini jambo ambalo linachusha imani ya wengi kuhusu imani na dini na kufanya baadhi ya vijana kuacha kuhudhuria ibada huku wengine wakihamia kwingine. Ufisadi sio jambo geni miongoni mwa viongozi wa dini za leo. Vyombo vya habari vimeripoti kashfa nyingi za kifisadi zinazohusishwa na viongozi wa dini. Kashfa hizi zinazidi kufanya vijana na haswa waliopevuka kimawazo kutoshwa na dini kufanya maamuzi ya kufuata mikondo yao ya maisha.

Ken Walibora katika riwaya yake ya kidagaa kimemwozea, anaangazia suala la ufisadi unaoendelezwa na viongozi wa kidini anapodai kuwa baba yao Mtemi Nasaba Bora na Mwalimu Majisifu ambaye alikuwa kasisi, alihakikisha watoto wake wameelimishwa na misheni badala ya kuwasaidia watoto wa walala hoi. Haya yapo kwenye dondoo iliyo hapa chini ;

''*Majisifu alikuwa kaelimishwa na misheni kama nduguye mkubwa. Ingalikuwa kwake vigumu kwenda ng'ambo alikoenda kama si pandashuka za babake kasisi. Alitarajiwa kusomea ukasisi ili aandame nyayo za babake.''* (Uk *27*)

Wengi wanaosoma katika jamii ya leo ni vijana wanaohitaji msaada kugharamia masomo yao haswa ya juu. Imebainika kuwa vituko vya baadhi ya viongozi wa dini za leo kuwalipia watoto wao karo kwa kutumia matoleo na misaada ya waumini vinazidi kuwakera vijana wengi wanaozidi kushuku ile haki na usawa zinazohubiriwa na viongozi hawa.

### 4.5.8 Injili Kuwa Chombo cha Kujitajirisha

Tajiri ni mtu mwenye mali ya vitu halisia au pesa. Mtu yeyote anaweza kuwa tajiri labda kwa bidii yake ya kutafuta riziki au kwa kurithi mali kutoka kwa wazazi wake (TUKI 2012). Mojawapo wa watu matajiri duniani na hasa barani Afrika ni wahubiri wa madhehebu tofauti. Wahubiri hawa wametajirishwa na matoleo yasiyotolewa ushuru kutoka kwa washirika wao. Wengine huwatapeli washirika wao kwa kuwadanganya kuhusu miujiza bandia. Kulingana na shirika la habari za jamii nchini Tanzania ; *Jamii Forums* mnamo tarehe 18 Februari 2022, wachungaji/maaskofu/manabii wengi Afrika Mashariki wanamiliki maelfu ya hekari za mashamba, viwanda, mashule, mabanki, magari ya kisasa na mabilioni ya pesa kwenye akaunti zao za kibinafsi. Wengi wa ''watumishi hawa wa Mungu '' wamekuwa wakichukua nafasi ya taabu wanazopitia washirika wao na kuwatapeli mali yao kwa hadaa za kuwaombea na kuwafanyia miujiza bandia. Hili limefanya wahubiri hawa kuzidi kuwada kwa utajiri usiokadiriwa huku washirika wao wakizidi kumasikinika zaidi.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia jinsi wahubiri wanavyotumia neno la Mungu kujitajirisha kwa kujilibikizia mali kwao badala ya kutumia mali ya kanisa kusaidia washirika wenye mahitaji. Kwenye Gazeti la *The Patriot* linalosomwa na Michael, mwandishi wake anachambua kashfa ambazo zilihusisha wahubiri kama dondoo hii inavyofafanua ;

''*Yeyote aliyetaka utajiri wa haraka alikimbilia injili. Humo humo ndimo watu walitafuta wake na hata wanawake. Makanisa yalianzishwa kwa haraka na kugawanyika kwa haraka kila mmoja akitafuta riziki yake. Imekuwa ni vigumu kwa yeyote kujua ni lipi kanisa bora na ni lipi si bora. Makanisa yote yalishindana yakivutana huku yakilaumiana.'' (Uk 220)*

Utajiri wa wahubiri pia unasisitizwa na Michael anaposema kuwa wana utajiri mwingi kwa kutenda mengi tu asiyoyataja. Usemi wa Michael unadhihirika kwenye dondoo iliyo hapa chini ;

''*Kwani ni mimi peke yangu ? Wahubiri wanafanya mangapi kwa jina la Yesu na wanazidi kuendelea ? Ndio wenye magari bora siku hizi. Ndio wenye nyumba za bei. Ndio wanaosomesha katika skuli za ghali. Na ndio wanaojilimbikizia pesa benki. Alijisemea kimoyomoyo huku akinywa soda ya sprite akingojea nyama ya kuchoma pale Nairobi West madukani.''. (Uk 163)*

Imebainika kuwa injili kutumiwa na baadhi ya viongozi wa kidini kama chombo cha kujitajirisha sio jambo geni katika jamii.Vijana wa karne ya ishirini na moja wameyashuhudia haya ya viongozi wa kidini kutumia dini kama chombo cha kujitajirisha na hivyo basi kuambaa masuala ya kidini.

**4.5.9 Wahubiri Kuishi Maisha ya Starehe na Anasa kwa Gharama ya Matoleo na Misaada.**

Starehe ni hali ya kuwa na amani na utulivu bila shida. Anasa ni hali ya kuwa na starehe na raha nyingi. Kwa binadamu yeyote kuishi maisha ya starehe na anasa ni lazima awe na pesa kwa wingi. Miaka ya hivi karibuni, wahubiri wa neno la ' Mungu' wamekuwa msitari wa mbele kutapeli waumuni wao ili kuishi maisha ya starehe, pia wahubiri hawa wanaitisha misaada kutoka ng'ambo wakitumia jina la maabadi yao wenye mahitaji na kuitumia kujifaidi wenyewe. Wahubiri hawa wamekuwa wakiishi kwenye mitaa ya kifahari, kuvalia mavazi ghali kutoka ng'ambo na pia kuendesha magari mazito yenye kutumia mafuta kwa wingi.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia jinsi wahubiri wengi wanavyoishi maisha ya starehe na anasa huku waumini wao wakiishi maisha ya uchochole. Habwe anawaangazia wahubri kama vile Askofu Joshua na mke wake Kasisi Lona pamoja na Boribori na mke wake Judy viongozi wa kanisa la Bethany wanavyoishi maisha ya kifahari kwa gharama ya matoleo na misaada inayolenga kuwasaidia waumini wenye mahitaji ya kuwaauni maishani. Kulingana na Habwe, Boribori alipenda kuvalia kispoti, suti kutoka *Italia*, miwani kutoka *Ujerumani*, tai zake ilibadili rangi kama kinyonga kutegemea unaziangalia kutoka wapi. Boribori alikuwa na gari la *Prado* lililopambwa kwa pazia maalum na kuendeshwa na dereva aliyestaafu kutoka jeshi huku Boribori akibebwa upande wa kushoto. Mhubiri Boribori aliishi kwenye jumba lililosimama kwa shamba la ekari mia mbili. Kwenye shamba hili mlikuwa na farasi na miti kwa wingi kupafanya mahali hapo ahera duniani. Mlikuwa na wafanyikazi wengi kwenye jumba lililotamba kwenye nusu ekari lililojengwa na waashi kutoka *Israeli*. Vyuma vya jumba hili vilitoka *Ujerumani* na vigae vya sakafu vilitoka *Ufaransa* na milango yake kutoka Kisiwa

cha *Pate*. Maandishi ya jumba hili yalichorwa na alfabeti za *Kiarabu*. Kwenye maegesho mlikuwa na magari sita. (Uk 222). Hali hii ya anasa na starehe ni suala la kawaida tu miongoni mwa makumi na makumi ya viongozi wa dini za leo. Vijana wa jamii ya leo waliopevuka na kusoma hawana stahamala tena kugharamia anasa za wahubiri hawa na hivyo basi ili kuhepa mifarakano nao, wanazidi kufuata mitazamo yao ya maisha na kujiepusha na masuala ya dini.

### 4.5.10 Viongozi wa Kidini na Waumini Kuhusishwa na Uganga na Mapepo

Uganga ni kazi ya kutibu magonjwa haswa kwa kutumia mitishamba. Mapepo ni roho chafu za mashetani zinazowaingia watu ili kuwatesa kwa magonjwa na mateso anuwai. Mapepo yanapoingia ndani ya mtu humfanya kutoroka nyumbani na kukimbia huku na kule huku akipayuka maneno yasisokuwa na msingi. Dini za ulimwengu haziruhusu waumini wake kujihusisha na mapepo na uganga ingawa haya hufanywa na waumini hawa kwenye siri. Habari zisiziominika ni kuwa wahubiri mashuhuri wamefumaniana kwa kushtukia na washirika wao usiku wa giza wakitafuta nguvu za kujinufaisha ugangani. John Habwe kwenye riwaya yake ya *Paradiso* anaangazia masuala ya mapepo na uganga kwa wahusika mbalimbali wanaoaminika kuwa watumishi wa Mungu wa kweli. Kwa nyakati tofauti, inadaiwa kuwa Askofu Joshua na mke wake Lona walikuwa mapepo waliotangatanga usiku huku wakiwasumbua waliolala kama ilivyo kwenye dondoo hii ;

*‘‘Lona na Joshua walishakuwa mapepo na walitangatanga dunia wakisumbua watu walalapo.’’ (Uk 136)*

Pia Musa anapokuwa na wendawazimu anawalaumu Joshua na Lona na kuwaita mashetani pale anaposema yafuatayo ;

*‘Nyinyi ni shetani. Ati wahubiri ? Wahubiri gani nyinyi ? Nyinyi ni laghai. Mwaiba. Mwalazimisha. Mwaongopa. Mwaua. Huku wataja Yesu. Shetani wakubwa nyinyi. Msitaje jina la Bwana bure. Kwendeni huko !’ (Uk 75)*

Vile vile, mwandishi huyu anamwangazia Michael ambaye baada ya kutafuta msaada wa ugonjwa aliokuwa nao kwenye maombi na hosipitalini, jamaa zake wanampeleka kwa mganga

wa kienyeji aitwaye Kabwere. Hii ni kinyume na imani ya Michael aliyetumainia Mungu kwa uponyaji. Na kwa vile lisilo na budi hutendwa, inabidi Michael kukubali kutibiwa na mganga. Haya yanadhihirika kwenye maneno ya Mganga Kabwere hapa chini ;

''*Nitawapa dawa ya kunywa. Baada ya siku nne uvimbe alo nalo utapotea. Uvimbe huo umesababishwa na majini. Majini hayo hayo ndiyo yaliyomnyonya damu. Hii ndiyo sababu amekonda hivi… itabidi mlale maana kubadili hicho kivimbe hadi miguuni hufanywa usiku wa manane''*. Kabwere alisema (uk 17).

Kwa mujibu wa nukuu zilizo kwenye sehemu hii tunapata kuwa baadhi ya viongozi wanaosifika katika masuala ya dini wamehusishwa na mapepo na majini na kutilia maji wito wao wa kutumikia Mungu. Habari hizi zinazidi kufifisha imani za kidini za vijana wengi na haswa walio na upevu wa mawazo. Baadhi ya vijana athirika wamelazimika kuhama au kuchoshwa na dini hadi kufikia uamuzi wa kufuata mikondo yao ya maisha isiyohusishwa na dini kwa vyovyote vile.

**4.5.11 Unafiki wa Matendo Miongoni mwa Wanadini**

Unafiki ni hali ya kutenda au kuwa na mienendo iliyo kinyume na matarajio ya jamii fulani au kwenye mazingira fulani. Pia ni hali ya mtu fulani kujifanya kuwa ni ' mwema ' au ' bora ' kuliko wengine. Pia inaweza kuwa hali ya kutenda mema fulani anapotazamwa na wengine lakini usiku wa shetani anajiingiza kwa vitendo viovu vilivyo kinyume na maadili ya jamii. Katika jamii ya waumini, kuna wale wanaojipendekeza kwa wengine kuwa viumbe safi wasio na hatia ilhali vitendo vyao vimejawa na uovu usiomithilika.

John Habwe anaangazia unafiki wa kidini katika riwaya yake ya *Paradiso* kupitia maneno ya mchungaji Michael ambaye katika mahubiri yake anakemea wale wanaojifanya wameokoka ila vitendo vyao ni kinyume na imani ya wokofu na kuwa wanayoyapinga ndiyo wanayotenda. Haya madai yanajitokeza kwenye mahubiri ya Michael kama ilivyo hapa chini ;

'*Yesu aliwashutumu mafarisayo kwa ajili ya unafiki. Mafarisayo walizoea kushtumu watu hali yake wanayoyapinga ndiyo wafanyayo. Mafarisayo wale wale ndio walioshughulika kuwaleta watu kwa Mungu na pia ndio waliowatoa.'' (Uk 55-56)*

Michael alifananisha vitendo vya jamii na vile vya Sodoma na Gomora zilizoangamizwa na Mungu kwa moto huku akiwahimiza waumini wake kurekebisha mienendo yao kama wangeendelea kumhubiri Bwana na kumfanyia kazi.

Ken walibora anaangazia unafiki katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea* kwa kurejelea yaliyomfisha moyo kijana Mwalimu Majisifu aliyeenda ng'ambo kusomea ukasisi ili kuandama nyayo za baba yake. Baada ya Majisifu kukagua dini kwa undani alitambua kuwa matendo yote maovu hutendwa kwa jina la "*Mungu*" na akaghairi nia yake kama ilivyodokezwa katika nukuu ifuatayo ;

"…*Alitarajiwa kusomea ukasisi ili aandame nyayo za babake. Lakini alipofika huko lipo lilimchusha moyo akatoshwa na dini. Dini kwake ilikuwa kasumba iliyoulewesha umma ukalewa chakari na kupepesuka.'' (Uk 27).*

Kisa hiki kinadhihirisha namna dini zi livyojawa na wanafiki huku wakijifunika ngozi za kondoo ilihali mioyoni mwao ni chui wauaji na waongo wakubwa hali zinazodhihirika kwa matendo yao.

Wakati wa enzi za giza, waumini walifuata chochote walichoambiwa na viongozi wao wa dini. Hakuna yeyote angeuliza swali kwani viongozi hawa walidhaniwa kuwa karibu na Mungu. Hata mmoja angepatikana akifanya vituko vya kishetani hakuna yeyote angemtupia mnong'ono kwa hofu ya kupatwa na adhabu kutoka kwa Mungu. Hata hivyo, unafiki wa kidini miongoni mwa waumini na viongozi wao unazidi kuongezeka katika jamii ya leo jambo ambalo linazidi kuporomosha imani ya wengi kila uchao na haswa waumini vijana. Vijana wengi wasomi na waliopevuka wanauliza maswali ya wazi kuhusu unafiki huu wa matendo na maneno na wanapokosa jawabu mwafaka wanaamua kujiepusha na masuala ya dini na kufuata falsafa zao kuhusu maisha jambo ambalo linazidi kuwatia kiwewe viongozi wa dini kuhusu madhehebu ya kesho.

### 4.6 Athari za Utamaushi wa Kidini kwa Vijana

#### 4.6.1 Vijana Kuchoshwa na Utaratibu wa Maabadani.

Maabadi ni mahali popote pa kufanyia ibada kama vile hekalu, kanisa au msikiti. Pia ni sehemu au eneo maalumu lililojengwa ambalo mtu au kundi la watu hukutana kufanya ibada au kujifunza masomo ya dini. Hata hivyo mnamo miaka ya hivi karibuni kumeibuka madhehebu ambayo hayafuati utaratibu wowote wa kufanya ibada zao kwa tetezi kuwa ibada inapaswa kuongozwa na Roho Mtakatifu. Hali hii imechosha vijana wa karne ya 21 na baadhi yao kuacha kuhudhuria ibada zenyewe na badala yake kujihusisha na starehe zao siku zilizotengwa za ibada. Suala hili la vijana kuchoshwa na taratibu za ibada limekuwa likiangaziwa na waandishi tofauti waliobobea na wale chipukizi.

John Habwe Katika riwaya ya *Paradiso*, anamwangazia kijana Kyalo aliyeichukia dini tangia akiwa kijana, sala za dini zilimchosha na aliona tu watu wengi walijihusisha na dini tu kwa sababu ya dhiki. Kyalo alichukia dini kiasi kwamba hata baada ya kuoa mke wake Salome alimwona mjinga kwa kujishughulisha na hadaa za wahubiri. Madai ya Kyalo yanadhihirika kwenye dondoo ifuatayo ;

'…*Kyalo hakupenda masuala ya dini. Tangu alipozaliwa hakuwa amekwenda kanisani. Hakuona haja yoyote ya kujidhiki na sala ndefu ambazo zilichosha. Hakupenda hasa sala za kelele. Alinona kuwa mke wake alikuwa mjinga kwa kujishughulisha na hadaa za wahubiri'* (uk49)

Kutokana na utafiti huu ni dhahiri shahiri kuwa Kyalo, anayewakilisha baadhi ya vijana katika jamii hakupenda kelele nyingi zilizopigwa na waumini wakati wa ibada na hivyo basi akafanya maamuzi ya kujiepusha na masuala ya dini. Hata alipokua na kuwa na familia msimamo wake ulibaki pale pale ; masuala ya dini haikuwa moyoni mwake kamwe.

#### 4.6.2 Vijana wa Kike Kukataa Kuolewa na Wahubiri.

Ndoa ni muungano kati ya watu wawili au zaidi unaokubaliwa na kuheshimiwa na jamii. Tukio la kuanzisha ndoa linaitwa harusi. Kabla ya ndoa, kuna kipindi cha uchumba ambapo watu hao wawili waliokubaliana wanachunguzana tabia na kujifunza au kujuana zaidi. Katika tamaduni

nyingi duniani, uhusiano huu huwa ni kati ya mwanamume na mwanamke ila miaka ya hivi karibuni kumekuwa na msukumo wa jamii fulani hasa kutoka *Ulaya* na *Marekani* kufanya ndoa ya watu wa jinsia moja. Katiba ya Kenya *kifungu cha* 4 *ibara ya* 9 kila aliyefikisha miaka kumi na nane ana haki ya kuolewa au kuoa na kuwa na familia. Hata hivyo, ndoa haipaswi kuwa ya lazima na kila mmoja anapaswa kujichangulia mchumba amtakaye. Miaka ya hivi karibuni ndoa imekumbwa na nyufa ambazo zinatishia kusabaratisha taasisi hii iliyoasisiwa na mababu zetu kabla ya karne ya ishirini na moja. Linalotilia msumari moto kwenye kidonda ni kuwa hata ndoa za wahubiri na viongozi wa dini zimekuwa na atiati na migogoro isiyokoma jambo ambalo linawafanya vijana na hasa wa kike kuwa na hofu ya kuolewa na viongozi wa dini. Katika riwaya ya *Paradiso*, kijana wa kike Nice ambaye pia ni bintiye Askofu Joshua na kasisi Lona wa kanisa la *New Jerusalemu*, anakataa katakata pendekezo la wazazi wao kuolewa na mhubiri Michael. Maisha ya unafiki wa kidini aliyoyaona na wazazi wake. Nice alikata kauli ya kutoolewa na mhubiri liwe liwalo kama inavyoelezwa na dondoo iliyo hapa chini ;

*'… Joshua na Lona walikaa hapo kumkabili Nice kuhusu pendekezo lao la kuolewa na Michael. Bila kificho Nice aliwaeleza hawezi. ''kwa nini mnitafutie mama, mama ?''. ''Hebu sikiliza mama, huyo mume ni kufu yako, ni mtu wa dini na ni rika lako'' alisema Lona…'' Najua ni mtu wa dini, lakini mimi mama si mtu wa dini'' Nice alisema kwa maringo'. (.uk 73)*

Usiku mzima Askofu Joshua na mkewe walimkorofisha binti yao angalau abadili msimamo wake na kukubali matakwa yao lakini Nice alibakia kwenye msimamo wake wa kutoolewa na mtu wa dini tena mhubiri. Nice alitamani kuachiwa uhuru wa maamuzi yake kama ataolewa au la. Alihofia kuolewa na mtu wa dini kwani alikuwa ameshuhudia mengi kwenye ndoa ya wazazi wake licha ya kuwa watumishi wa Mungu. Hata baada ya wazazi wa Nice kuwa na hasira na kumtishia binti yao kutafuta wazazi wengine endapo angekataa pendekezo lao la kuolewa na mhubiri Michael, Nice alisimama kidete kuwa yeye sio mtu wa dini na hataki kuolewa na mtu wa dini.

Kwa vile fasihi ni kioo cha jamii, utafiti huu unatambua Nice ambaye ni kiwakilishi cha vijana wa kike kwenye jamii ya karne ya ishirini na moja wanaodinda kuolewa na wahubiri kwa hofu

ya kutiwa pingu na dini licha ya kulelewa na jamii ya viongozi wa dini. Wao wangetaka kuwa huru kutafuta waume zao bila kulazimishwa na wazazi wao.

### 4.6.3 Vijana Kushuku Uwezo wa Mungu.

Kila binadamu duniani huamini kuwa kuna kiumbe mwenye nguvu na uwezo kumliko. Kiumbe huyu ndiye mpaji wa uhai na ndiye ajuaye uhai huenda wapi baada ya viumbe kufikwa na mauti. Jamii nyingi humpa kiumbe huyu majina tofauti ikiwemo *Mungu*, *Maulana*, *Mola*, *Rabana Karima* miongoni mwa majina mengine. Kiumbe huyu hudhaniwa na jamii ya mwanadamu kuwa na nguvu nyingi na uwezo wa kuamua hali ya baadaye na hatima ya mwanadamu huyu na hivyo mwanadamu humcha na kumheshimu mara nyingi. Kwa imani, kiumbe huyu hukimbiliwa hasa wakati kuna ugumu wa hali kwa imani kuwa ataleta suluhu na hali ya utulivu. Kwenye vitabu vitakatifu, *Mungu* hutajwa kama ngome ya kukimbiliwa wakati wa haja. Hata hivyo, vituko na kashfa miongoni mwa viongozi wa kidini kwenye madhehebu tofauti miaka ya hivi karibuni, zimefanya waumini wengi kushuku uwezo wa' Mungu' wa kubadili hali zikiwa na utata. Vile vile, matatizo yanayozidi kuongezeka kila uchao yakiwemo magonjwa, ajali, mauti na majanga ya kila siku yanazidi kufanya waumini wengi kushuku uwezo wa 'Mungu' wa kutuliza hali hizi. Vile vile, jamii inatarajia maombi na ibada zinazofanywa na waumini kila siku zifanye Mungu atulize hali ya mizozo iliyomo kwenye madhehebu mbalimbali.

Ken Walibora katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea*, anamrejelea kijana wa kike Imani ambaye anashuku uwezo wa Mungu aliyeruhusu kufikwa na dhiki iliyompata pale nyumbani aliponusurika kuchomwa na wenye wivu. Madai ya Amani yanadhihirika kwenye dondoo hii;

*'Basi niliponusurika kuteketezwa nilitoka nikatazama mbingu na kuwaza sana. Kwa nini Mungu aliruhusu dhiki kama hiyo kunikusa*?' (uk58-59)

Maneno ya Imani ni kuwa Mungu mwenyewe hakuwa na uwezo wa kumlinda na hali ya maadui kutaka kumteketeza kwani hangekuwa na uwezo angemlinda kutokana na wahuni waliochoma nyumba yao na hangeruhusu wafike kwa boma lao.

Mount Kenya University

John habwe katika riwaya yake ya *paradiso* anamrejelea kijana wa kike lydia ambaye aliamini kuwa ana uwezo wa kufanya mambo mengi na kuwa mungu yuko tu anapokuwa hajiwezi. Haya yote yanajitokeza katika dondoo ifuatayo;

''*Lydia haya ya dini yalimfutu. Hakuyafuatilia kwa karibu. Angewezaje huku mama yake ndiye huyo? Au ni kweli walivyosema mwana huiga kisogo cha nina. Lydia alijua kuwa Mungu yuko anapokuwa hajiwezi. Pale unapoweza unayafanya mwenyewe''(uk97)*

Utafiti huu unatambua kuwa kwenye mawazo ya Lydia ni kuwa Mungu anapaswa kuingililia kwa maisha ya mtu tu pale ambapo mtu huyo amelemewa na pale ambapo mtu huyo anaona anaweza basi anapaswa kujishughulikia. Yaani sio lazima mtu kutegemea Mungu kwa kila jambo.

### 4.6.4 Vijana Kukataa 'Kuokoka' na Kuingia katika Anasa.

Kuokoka ni kitendo cha kutoka sehemu moja iliyo na hatari na kwenda sehemu nyingine ambayo ni salama. Kulingana na *Samuel Mtimbike* (2022), kwa dini ya Kikristo, kuokoka ni kuitii injili ya Bwana Yesu na kisha kubatizwa katika ubatizo sahihi ambao ni wa maji mengi na kwa jina la Yesu na kupokea kipawa cha Roho mtakatifu na kisha kuishi maisha matakatifu kwa kufanya mapenzi ya Mungu. Kulingana na dini ya Kiisilamu, waliomkubali *Mohamad* na kufuata amri zake wamekwisha okoka na watapata Bustani zipitazo mito kati yake. Humo watadumu milele. Kulingana na mafundisho ya dini, wokovu ndio zawadi kubwa anayoweza kupata mwanadamu kwani inamhakikishia uzima wa milele Paradiso. Wokovu huu unahitaji kila muumini kuishi maisha ya utakatifu yasiyo na dhambi kulingana na mafundisho ya dini yake. Hata hivyo, jinsi siku zinavyosonga ndivyo waumini wengi na haswa vijana wanavyozidi kukaidi injili ya wokovu na badala yake kujiingiza kwenye ''dhambi'' za kila aina zikiwemo ulevi, ukware, utovu wa maadili, anasa na starehe za kila aina kinyume na mafundisho ya dini zao. Kisa na maana, wanaowaongoza kwenye mafundisho haya ya kidini wanayatenda maovu haya wazi bila woga wa adhabu ya Muumba wao.

Katika riwaya ya *Paradiso*, John Habwe anamrejelea kijana wa kike Nice bintiye Askofu Joshua na kasisi Lona aliyetoshwa na wokovu wa wazazi wake na kuzamia starehe zake za maisha kule *New York*. Salamu za Nice zililetwa nyumbani na Bwana Njenga aliyekutana naye kule *New York* katika shughuli zake za ukasisi. Bwana Njenga alipojaribu kumpa Nice habari za Yesu, Nice alimkumbusha kuwa baba yake ni mhubiri na kuwa hakuweza kumuokoa. Mwandishi anasema kuwa Nice alikuwa amejizika zii katika ulevi na matembezi. Ithibati ya utafiti huu imo katika nukuu ifuatayo ambayo ni mazungumzo ya Bwana Njenga na kijana wa kike Nice bintiye Askofu Joshua na Kasisi Lona;

> *'Nice alikuwa amesahau kisomo chake. Alijizika ziii katika ulevi na matembezi…. Well, nilitaka kukuuliza unakaa wapi*? *Unaa…Yaani nilitaka umkubali Yesu''…''Sikiza*. *Baba yangu ni mhubiri*. *Hakufaulu kuniokoa*. *Wewe hutafaulu*. *Ninakoishi na nikifanyacho yakuhusu vipi*?''*Baada ya mjadala huu kati ya Nice na Bwana Njenga, Nice alichomoka nje bila kuaga na suruari yake ya kubana ambayo kuivua kwake alikuwa lazima angesaidiwa'.* (uk128)

Utafiti huu ulitambua kuwa kijana wa kike Nice, alikuwa amechoshwa na ukosefu wa uaminifu kwa wazazi wake licha ya kuwa wao walikuwa watumishi wa Mungu na badala yake akazamia kuhamia *New York* alikoishi maisha ya ulevi na starehe alizotaka mwenyewe. Huu ndio uhuru alioutafuta maishani mbali za wazazi wake waliookoka.

**4.6.5 Vijana Kuzinduka na Kuuliza Maswali Kuhusu Dini Hadharani.**

Kuzinduka ni kitendo cha kutoka katika bumbuazi au kutoka katika hali ya kutoelewa jambo. Mtu yeyote anaweza kuzinduka kimawazo na kuwa na falsafa mpya kuliko aliyokuwa nayo hapo awali. Katika kipindi cha zama za giza, binadamu aliacha hali ya kimaumbile na jaala kuchukua mkondo wake bila kutia juhudi zozote za kudhibiti changamoto zilizotesa kiumbe huyu. Hata hivyo, baada ya kipindi cha ufufuo, binadamu alianza harakati za kujikomboa kutoka sirisiri za utumwa zilizomfunga kwa miaka nyingi zikiwemo zile za kidini, uchumi, teknolojia na ujinga wa kutosoma. Kiumbe huyu alianza kutafuta maarifa na ujuzi ambazo zingempunguzia taabu alizokubana nazo siku nenda siku rudi. Upande wa kidini, watu walifundishwa mafunzo na itikadi kali kwamba ili kumfikia Mungu ni lazima muumini yeyote apitie kwa *Papa mtakatifu*. Kulingana na *Ellen* G. *White* (2023), mwanzo wa utawala wa *Kanisa la Rumi* ulikuwa mwanzo

Mount Kenya University

wa utawala wa giza na jinsi uwezo wa kanisa ulivyoogezeka ndivyo pia hali ya giza ilivyoongezeka. Anasema kuwa Imani ya wengi kuwa Yesu mwana wa Mungu ndiye mwazilishi wa kanisa iligeuzwa na badala yake papa na maasikofu aliowapa mamlaka kuadhimishwa.

Papa alipaswa kuheshimiwa na kila muumini na kukosa kumtii na kufanya mapenzi yake kukawa adhabu kali ya mwilini na rohoni. Dhambi ilifunikwa na vazi la utakatifu na hapo ubaya wa kila namna ukatokea kwa ajili ya kuacha kuzifuata amri za Mungu. Waumini walinyamazia masuala mazito bila kuuliza chochote kwa hofu ya kuadhibiwa. Hata hivyo, mnamo mwanzoni mwa karne ya ishirini na moja, kumeibuka kizazi ambacho kimeziduka kiasi cha kuuliza viongozi wa kidini maswali ya moja kwa moja hasa mahali wanapoona sitofahamu. Hii ni kwa sababu ya kugundua dhahiri shahiri kuwa viongozi hawa wa kidini ni binadamu wa kawaida tu na wana vituko kama binadamu yeyote yule. Viongozi hawa wanachukiana, wanagombana hadharani, wanachochea washirika wao kupigana na wanaoneana wivu wao kwa wao kama binadamu wa kawaida afanyavyo tu.

John Habwe kwenye riwaya yake ya *Paradiso*, anarejelea kiongozi wa kikundi cha vijana pale kwenye kanisa la *Bethany* lililoongozwa na kasisi Michael. Uhusiano wa Michael na Patricia na kukosa kuwa mwaminifu katika ndoa yake na Lydia, kuliwapa vijana nafasi ya kuzinduka na kuuliza hadharani kuhusu matumizi ya misaada iliyotoka ng'ambo na usimamizi wa nasari iliyokuwa chini ya kanisa jinsi inavyojitokeza kwenye nukuu iliyo hapa;

''*Tayari mwanya uliingia Bethany. Kuna kikundi kilichoona hakikufaidi vizuri pale Bethany. Kikundi hiki kiliongozwa na Kariuki. Kariuki alikuwa kiongozi wa vijana kaika kanisa la Bethany. Kikundi cha vijana kilidai misaada yote iliyotoka ng'ambo ilikuwa katika mikono ya wachache*.?'' (uk153.)

Utafiti huu unatambua kuwa vijana wa jana ni tofauti na wale wa sasa kwani wale wa sasa hawana woga tena na pindi waonapo jambo lenye utata wanalikashfu moja kwa moja. Ndio maana Kariuki, kiongozi wa vijana katika kanisa la *Bethany* anaongoza vijana wenzake kuuliza maswali peupe bila woga wowote kinyume na ilivyokuwa hapo awali.

Mount Kenya University

### 4.6.6 Vijana Kuacha Kuhudhuria Ibada.

Ibada ni kitendo chochote kinachofanywa kuonyesha unyenyekevu wa hali ya juu, utiifu, heshima, shukrani na utukufu aidha kwa Mungu au kitu kilicho na mamlaka makuu kuliko binadamu. Dini zote duniani huwa na ibada zinazofanyiwa mahala teule labda kwenye majengo ya kifahari au kachara, chini ya miti, mapangoni, juu ya miamba au hata misituni. Maabadi haya huheshimiwa na huwa muhari kila mmoja katika jamii ahudhurie ibada kulingana na muda na wakati uliotengwa. Hata hivyo, vijana wa karne ya ishirini na moja wamekuwa na mahudhurio duni ya ibada kwa tetesi kuwa matakwa yao hayatiliwi maanani na viongozi wa maabadi na haswa wazee. Kulingana na Rais Dallin H. Oaks (2021),

kuna wasiwasi miongoni mwa viongozi wa kidini kwani kuna mahudhurio duni ya ibada kwenye majengo ya masinagogi, misikiti au mashirika mengine ya kidini na kuwa mahudhurio haya yameshuka kwa kiasi kikubwa. Vijana haswa waliokwea kwenye kiwango fulani cha masomo wanazidi kuwa na mahudhurio duni ya ibada. Hii ni baada ya viongozi wa kidini kujihusisha na kashfa za kila aina hadharani zikiwemo mipango ya kando, ufisadi na matumizi mabaya ya mali ya maabadani.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso*, anarejelea mahudhurio duni ya vijana katika kanisa la *Bethany* baada ya kiongozi wa kanisa hili Michael kupatikana na kashfa ya uhusiano wa nje ya ndoa na Patricia licha ya kuwa na mke wake mwanadini Lydia. Haya yanadhihirika katika maneno yafuatayo;

*‘’Japo bado kulikuwa na waumini lukuki Bethany hasa wale waliofuata miujiza, kundi kubwa lilinyofoa na kujiondokea. Ahadi zilipotolewa bila mafanikio hapakuwa na sababu ya kuendelea kuning’inia Bethany.Kundi la vijana tayari lilijibambua kama gome la gogo.*’’(uk160).

Utafiti huu unadhibitisha madai kuwa vijana wanazidi kuchoshwa na masuala ya dini na wanazidi kuyakimbia na kujipa shughuli zao. Hii ni baada ya vijana hawa kutambua kuwa viongozi wa kidini wanaowaongoza wamejawa na kashfa chungu nzima. Wanaamua kujiondoa mmoja baada ya mwingine.

**4.6.7 Vijana Kuwa na Ukakamavu wa Kudharau Watumishi wa Mungu Peupe.**

Watumishi wa Mungu ni viongozi waliotwikwa mamlaka ya kuongoza ibada katika madhabau ya waumini. Kila dhehebu duniani huwa na viongozi wake wanaopaswa kuheshimiwa na kusikizwa kwani ndio hutwikwa jukumu la kufundisha mafunzo ya kidini kulingana na mila na itikadi za dini husika. Vile vile, watumishi hawa wa Mungu wanapaswa kujiheshimu na kuwa waangalifu kwa maneno na matendo yao kwani chochote wanachosema au kutenda hadharani hutiwa kwenye mizani na waumini walio chini yao.

Hata hivyo, watumishi hawa wa Mungu wanazidi kujihusisha na vituko vya kila aina ikiwemo kulaghai waumini kwa jina la Mungu, kufanya miujiza bandia, kuwa na mipango ya kando na kashfa za pesa miongoni mwa kashfa zingine. Vituko vyao vinazidi kuwapunguzia heshima na kufanya waumini na haswa vijana waliozinduka kuwadharau hadharani. Kulingana na *Ellen* G *White* (2023), vijana na watoto wanazidi kuonyesha dharau kwa kazi ya Mungu na watumishi wake kutokana na masengenyo wanayopata kutoka kwa wazazi wao. Hili limefanya kuwa vigumu kudumisha utaratibu na kuwatawala kwa busara vijana walio chini ya uangalifu wao. Vijana hawa hawaongopi tena kuwatemea maneno mazito mazito watumishi hawa wa Mungu na pia kudharau sheria za Mungu kinyume na matarajio ya mafundisho ya dini.

John Habwe katika riwaya yake ya *Paradiso*, anawarejelea vijana wanafunzi wa shule ya upili ya Alliance Girls wanaodharau mtumishi wa mungu na mke wake Michael, Lydia. Hii ni baada ya vijana hawa kughudua kuwa Patricia analea mimba ya mhubiri na mume wake mwalimu wao. Walianzisha dharau kwa mwalimu wao kwa kutupa vijikaratasi hapa na pale kukashfu vitendo vya mume wa mwalimu wao aliye mtumishi wa Mungu kwenye kanisa la Bethany. Idhibati ya dharau hili ipo kwenye dondoo ifuatayo;

‘‘*Hata ilipojulikana wazi kuwa Patricia analea mimba, shule nzima hata wanafunzi walijua. Lydia amebakia pale na rafiki wachache. Walimu wengi ni wa kumsengenya akipita. Sasa yeye ameamua akae kando.*’’ (*uk 204*)

Kwa mujibu wa nukuu hii inabainika wazi kuwa wanafunzi wametamaushwa na vitendo vya mume wa mtumishi wa Mungu na pia mwalimu Lydia ambaye anakumbana na hali nzito pale shuleni kwani hana uso wa kutazama wanafunzi hawa wanaosema ukweli wa jinsi hali ilivyo kuhusu ndoa yake na mume wake Michael. Anapunguza maneno yake na kuondoka shuleni pindi tu vipindi vyake vya masomo vinapokamilika.

### 4.6.8 Vijana Kukataa Kazi ya Mungu Peupe.

Kazi ya Mungu ni kitendo cha kutoa huduma iliyo au isiyo na malipo kufanya kazi ya Mungu. Kila dhehebu huwa na nafasi yake ya utumishi wa kazi ya Mungu kulingana na kanuni zao. Kwa yeyote kuwa na nafasi ya utumishi huu anapaswa kuwa na elimu fulani ya kithiolojia kulingana na kitengo ambacho angependa kuegemea. Ili kupata nafasi ya kutoa huduma husika ni lazima kufuata masharti fulani yaliyowekwa kulingana na kanuni za dhehebu husika. Katika karne ya 21, idadi ya vijana katika utumishi wa Mungu imepungua jambo ambalo linazidi kutia wazee na viongozi wa madhehebu kiwewe kila uchao. Tafiti na maandishi mengi kwenye masuala ya dini zinadhirihisha kuwa vijana wanazidi kukataa utumishi wa Mungu na kuwa washirika tu wasiodhibitiwa kikamilifu na dini.

Kulingana na shirika la *Gogle* (2006), tafiti mbili zilizofanywa na kundi la *Barna* na *USA Today*, walipata kuwa karibu asilimia 75 ya vijana Wakristo wanaondoka kanisa baada ya shule ya sekondari. Hali hii imetokea kwa sababu vijana hawa wanatumia muda wao mwingi shuleni kunakofunzwa maadili yanayopinga Biblia. Vijana wengi hawana nafasi tena ya kuwaelimisha watoto wadogo kuhusu mafundisho ya dini zao na jukumu hili wameachia wazazi wao na viongozi wa kidini waliokomaa jambo ambalo linazidi kutia kiwewe kwa viongozi hawa kwani kuna hofu kuwa walimu wa dini wanapungua kila uchao kwani vitendo vya vijana hawa ni ishara ya kukataa kazi ya Mungu.

Ken Walibora katika riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea*, anamrejelea kijana Mwalimu Majisifu Majimarefu aliyefadhiliwa na Misheni kwenda ng’ambo kusomea ukasisi ili kurithi

viatu vya baba yake ya ukasisi. Majisifu anapoenda ng'ambo anaghairi mtazamo huu wa kazi ya Mungu na kuamua kuishi maisha yake yasiyo na uhusiano na kazi ya Mungu jinsi inavyojitokeza katika nukuu hapa chini;

'*Mwalimu majisifu alitarajiwa kusomea ukasisi ili aandame nyayo za babake. Lakini alipofika huko lipo lilimchusha akatoshwa na dini. Dini kwake ilikuwa kasumba iliyoulewesha umma ukalewa chakari na kupepesuka…. Aliona kwamba ingawa dini zote huhubiri Amani, udugu, na rehema, ila maovu na makuruhu mengi katika historia ya mwanadamu mathalan husuda, uongo, usongombwingo na vita yametendwa katika jina la Mungu. Kwa hivyo akaghairi nia ya kuwa kasisi'*. (*uk27)*.

Utafiti huu unatambua kuwa ingawa watumishi wa Mungu wana nia nzuri ya kurithisha utumishi huu kwa watoto wao, kuna mambo nyeti yanayotinga hamu ya vijana hawa kuendeleza azma ya wazazi wao. Licha ya kuwa kasisi na baba yake Mwalimu Majisifu angetamani mtoto wake aiendeleze kazi ya Mungu kwa kufuata nyayo zake, kijana huyu alighairi nia hii kwa kutambua kuwa dini imejawa na unafiki mwingi na matendo mengi maovu yanafanyika kwa jina la Mungu.

### 4.6.9 Vijana Kutafuta Miungu na Ibada Zingine.

Miungu ni jina linalojumlisha wahusika wanaoabudiwa katika dini mbalimbali kama wenye nguvu na enzi juu ya maisha ya mwanadamu. Tangu kipindi cha *Neolithic,* binadamu katika dunia wamekuwa wakifanya ibada za miungi tofauti kulingana na kipindi fulani cha mwaka. Kulikuwa na miungu ya wakati wa mavuno, wakati wa kiangazi, wakati wa mafuriko, baada ya majanga kutokea na kadhalika. Hata hivyo jinsi siku zilivyosonga ndivyo akili za waumini zilivyobadilika na kuelekeza ibada zao kwa Mungu mmoja kulingana na makubaliano. Kulingana na *Gasper Madumla* (2014), jinsi dunia ilivyosonga ndivyo ongezeko la dhambi lilivyozidi na kumfanya mwanadamu kugeukia katika aina mbali mbali za ibada na hapo kukatengenezwa aina kubwa tatu za ibada ambazo ni; ibada kwa Mungu aliye hai, ibada kwa miungu ya jadi, mizimu, matambiko na mashetani na ibada kwa mwanadamu, vitu, fedha na mali. Katika karne ya 21, baadhi ya wanajamii na haswa vijana wamejikita katika uhuru wa kuabudu chochote watakavyo zikiwemo anasa na starehe zao. Waandishi tofauti wamekuwa

Mount Kenya University

wakiangazia waumini wanaoamua kuabudu vitu tofauti na kutumia mitindo tofauti ya maisha kulingana na matakwa yao.

Ken Walibora kwenye riwaya yake ya *Kidagaa Kimemwozea*, anamrejelea Mwalimu Majisifu ambaye baada ya kuchoshwa na Mungu na ibada za maabadi aliamua kuwa na mungu wake 'pombe' na ibada yake ikawa 'ulevi. Madai hayo yanajitokeza kwenye dondoo iliyo hapa;

''…*lakini hatimaye alikuwa mwalimu tu wa shule ya upili. Na lau asingekuwa na wanaomjua wenye satua, asingalikuwa hata na ualimu huo. Mambo yake yalikuwa taibu hadi alipoanza kuabudu* '*Mungu' mwingine kwa himdi na twaa. Pombe ilikuwa mungu wake na ulevi ndio ibada aliyoipenda kwa dhati ya* moyo*''.* (*Uk28*).

Utafiti huu uling'amua kuwa hata baada ya kijana mwalimu majisifu kukua na kuoa mke wake Dora, alizidi tu na ibada yake bila hofu kwani aliamini kuwa huu ndio uhuru aliopaswa kuwa nao binadamu yeyote wa kuachiwa mwanya wa kufuata sera zake bila kuingiliiwa na yeyote.

Mwalimu Majisifu anakosa kuhudhuria mkutano wa kusherehekea uhuru wa taifa la Tomoko kwenye uwanja wa Sokomoko kisa na maana alikuwa ameenda ibada jinsi ilivyo kwenye maneno yafuatayo;

*'Majisifu mbona sikukuona mkutanoni*?'' *Bwana Mtemi alimuuliza nduguye hatimaye baada ya kimya cha kitambo kirefu…''Nilikuwa nimekwenda ibada kaka.*'' '*'Tembo itakuua ndugu yangu.Punguza ulevi bwana.Unautukanisha ukoo wetu mtukufu.Siku hizi hata naona aibu kukuita ndugu yangu. Niliambiwa jana kwamba ulilala mtaroni siku ile ya sherehe usiku kucha.Hii ni aibu bwana.Kumbuka marehemu baba yetu alikuwa kasisi ndugu yangu. Alikuwa akisema kwamba walevi hawataingia katika ufalme wa mbinguni''* (*uk93*.)

Utafiti huu ulitambua kuwa Mwalimu Majisifu alikuwa ametamaushwa na masuala ya kidini bado angali kijana kwa aliyoshuhudia yakifanywa na wanadini. Hili likamsukuma kujitafutia ibada yake ya ulevi tangia ujanani wake licha ya baba yake kumtaka awe kasisi kama yeye. Hivyo basi akahasi Mungu na Ibada za babake na kufanya maamuzi kuwa pombe ndiyo mungu wake wa kila siku.

## 4.7 Mapendekezo ya Waandishi John Habwe na Ken Walibora ya Kukabiliana na Udhanaishi wa Kidini kwa Vijana.

John Habwe na Ken Walibora wanapendekeza baadhi ya njia zinazoweza kutumika ili kujenga imani katika mioyo ya vijana kuhusu masuala ya dini kwa lengo la kupunguza ukataji wa tamaa



Mount Kenya University

unaojengekeka kwao kila uchao.  Baadhi ya mapendekezo yaliyomlikwa na waandishi hawa ni pamoja na shughuli za ibada kuendeshwa kwa utaratibu wa pole pole na uungwana. katika riwaya ya *Paradiso*, baada ya mhubiri Michael kutoka *Marekani*, alifika na maoni kuwa shughuli za kanisa zilifaa kuendeshwa kwa utaratibu wa pole pole na uungwana bila kelele na kucheza kwingi kama kwamba leo dini ni disko. (uk 97-98)

Pili ni kutumia maafisa wa polisi na askari kwenye sehemu za maabadi ili kutuliza ghasia zinapozuka miongoni mwa washirika. Hii ni kwa sababu uwepo wa maafisa hawa utawafanya vijana kuwa na imani kuwa wanaoazimia kuleta fujo kwenye sehemu hizi za maabadi watakuwa na hofu na hivyo kufanya ibada kwa utaratibu. Katika riwaya ya *Paradiso*, maafisa wa polisi wanafika kuzima fujo na kutenganisha vikundi vilivyokuwa vikipigana katika kanisa la *New Jerusalemu* ambapo watu kadhaa walikuwa wameumizwa kwenye vurumai zilizotokea. (uk77). Maafisa hawa hawa wa polisi ndio waliotumiwa kuchunguza kashfa ya biashara ya mihadarati na madini iliyoendeshwa katika kanisa la *New Jerusalemu* (uk 198).

Vile vile, katika riwaya ya *Kidagaa Kimemwozea*, askari wa Mtemi Nasaba Bora wanalazimika kuzima ghasia zilizokuwa na vita baina ya makanisa mawili yaliyopigana kadamnasi sokoni juu ya uwanja wa kujenga maabadi ambapo kama haingekuwa askari hao wanamakundi hawa wangeuana waangamizane (uk 93).

Njia ya tatu ni kutumia mahakama kutoa maamuzi ya ni wapi palipo na makosa vurugu zinapotokea. Katika riwaya ya *Paradiso*, ilibidi kanisa la *New Jerusalemu* kufungwa miezi minne kungojea mahakama kuamua ni nani anamiliki nini katika majengo ya maabadi(uk77). Mahakama pia inatumika kusikiza kesi kuhusu biashara ya ulanguzi wa mihadarati inayoongozwa na wa kanisa la mhubiri Boribori pale New Jerusalemu.Mahakama hii inatumika kumfunga Boribori na mkewe Judy kwa nia ya kusafisha magugu maabadani ili kujenga imani mpya kwa washiriki. (uk 217)

Njia nyingine ya kujenga imani ya kidini miongoni mwa vijana ni kurekebisha tabia na mienendo ya washirika iwapo wangeendelea kumhubiri Bwana na kumfanyia kazi. katika riwaya ya *Paradiso,* Mhubiri Michael anasisitiza kuwa endapo wanaodai kuwa wameokoka wangejitayarisha katika ulimwengu kwa maisha ya ahera hawana budi kurekebisha na kubadili mienendo yao kwa kuhasi mauaji, ubakaji, wizi, ufisadi na kashfa zingine zilizoitanishwa na waumini la sivyo walio nje watazidi kuambaa masuala ya dini. (uk 56)

Vile vile, waandishi hawa wanapendekeza kupunguza muda unaotumika kufanya ibada na kutumia lugha inayoeleweka na kila mwanaibada. Vijana wengi huchoshwa na muda mwingi unaotumika katika ibada haswa mahubiri. Kwenye riwaya ya *Paradiso*, mhubiri Michael wa kanisa la Bethany, alipunguza mahubiri yake kutoka saa moja hadi dakika kumi na tano. Anapoamua kutumia kiingereza, Bwana Kitwana huwa mkalimani wake ili kuwafikia watoto, wanawake, wanaume, vizee, wagonjwa na wazima walioujaa ukumbi wa Bethany. (uk 160) Pia, wazazi wanapaswa kuwaasa watoto wao wakiwa wadogo na kuwaadilisha njia ambazo wangefuata ili kukua kwa uangalifu usiotetereka. Hii ni kwa sababu mwalimu wa kwanza wa mtoto ni mzazi au mlezi wake na kuwa kwa asilimia pana mtoto hukua kulingana na mienendo ya mazingira aliyolelewa. Katika riwaya ya *Paradiso*, Patricia alikumbuka maneno alomweleza mamake Wanjiro alipopata mtoto wa pili. Patricia alionywa na mamake vikali dhidi ya kumvulia mtu yeyote nguo mpaka atakapoingia katika ndoa halali. Mama huyu alimfundisha bintiye kuwa asijipendekeze kwa mume yeyote kwani kujipendekeza kwa mwanamume ndiko kufukuzwa huko. (uk171-172) Mama huyu alimkumbusha bintiye kuwa yeye bado ni mtoto kwani hakuwa na uwezo wa kutenganisha haramu na halali.

'*Kwangu hutakuwa mtu mzima.Mtu mzima ni mimi mama yako niliyekuzaa na unayepagaza. Kama ungekuwa mtu mzima ungejua uharamu ulioko kutembea na mtu asiyekupenda akakutia mimba na kisha…'' Wanjiro alighafilika kumaliza'. (uk176)*

Wosia kama huu kwa vijana ungewaadilisha na kujenga misingi yao katika mafundisho ya kidini na hivyo basi kupunguza anasa, mipango ya kando na unafiki wa kidini miongoni mwa washirika na hivyo kuvutia vijana kwenye Imani yake.  Viongozi wa kidini na wahubiri wanapaswa

kubadilisha mkondo wa injili kutoka kwa matoleo ya kila siku na badala yake kuhubiri jinsi binadamu anapaswa kuishi na binadamu mwenzake.

Hii ni kwa sababu pasipo na haki na umoja wa washirika hata maabadi yenyewe hayataweza kusimama imara. Katika riwaya ya *Paradiso*, baada ya Mchungaji Boribori kufungwa jela, Nana aliyechukua mahali pake aliweka mkondo mpya wa injili. Injili yake ilitoka kwenye 'zaka na maendeleo' hadi kwenye 'kwenenda kwa haki na kupendana kwa majirani'. Kulingana na Nana, subira ilikuwa muhimu ili kupata ahadi za Bwana maanake Bwana Mungu alikuwa na saa yake na mikakati yake ya kufanyia mambo ambayo haikuwa lazima kwenda sambamba na ya wanadamu. Baadaye waumini walianza kuona ukweli katika injili ya Nana na baadhi ya waliokuwa wamegura walirejea na wageni kutoka ulimwengu na makanisa jirani wakaanza kufurika kwenye kanisa la *New Jerusalemu*. (uk 226) Hii ina maana kuwa waumini vijana wengi hukosa imani kwenye dini kutokana na matoleo ya mara kwa mara na endapo mkondo wa injili utabadilishwa watarejea maabadani kwa moyo wa dhati.

Mapendekezo yaliyo hapo juu yanaweza kutumika kupiga hatua kujitahidi kushughulikia kiwewe cha vijana kutamaushwa na mafundisho ya dini yanayojikita katika mafundisho ya maadili katika jamii. Utafiti kuhusu udhanaishi wa kidini na athari zake kwa vijana bado ni mchanga.Hivyo basi,mtafiti hawezi kujigamba kuwa ameangazia vipengele vyote vinavyotagusana na udhanaishi wa kidini. Hii ina maana kuwa bado kuna mwanya wa kuangazia suala hili nyeti katika jamii ya karne ya ishirini na moja. Kwa vile mtafii ameengemeza kazi yake kwa waandishi wa vitabu,anapendekeza nafasi ikipatikana tafiti zaidi za nyanjani zifanywe na watafiti wachanga na waliobobea kubaini ukweli ulioibuliwa na waandishi tofauti tofauti.

## 4.8 Hitimisho

Kulingana na utafiti uliofanywa ni ukweli usiofichika kuwa kuna masuala chungu nzima yanayofanya vijana watamaushwe na masuala ya kidini kila uchao. Kwa vile hamna lolote lisilo na athari zake,utamaushi huu una athari maridhawa kwa vijana hawa hali ambayo ikikosa

kutafutiwa suluhu mwafaka itakuwa na athari mbaya kwa masuala ya ibada za siku za kesho. Katika sehemu hii,tumechanganua baadhi ya mbinu za kukabiliana na udhanaishi wa kidini jinsi zilivyopendekezwa na waandishi John Habwe na Ken Walibora

Mount Kenya University

# SURA YA TANO

# MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.0 Utangulizi

Kwa jumla katika sura hii,hitimisho la utafiti litaangaziwa.Vile vile,muhtasari,matokeo, mchango pamoja na mapendekezo ya mtafiti yataangaziwa.

## 5.1. Muhtasari wa Utafiti

Utafiti huu ulilenga kuchunguza udhanaishi wa kidini miongoni mwa vijana katika riwaya

Za kiswahili. Riwaya zilizoteuliwa ni zile za *Paradiso* na *Kidagaa Kimemwozea* mtawalia.

Utafiti huu ulichunguza sababu zinazofanya vijana wa karne ya ishirini na moja kulegea kwenye imani na dini. Pia, utafiti huu ulichunguza athari za udhanaishi wa kidini kwa vijana husika na

hatimaye kuonyesha mapendekezo ya waandishi kuhusu suluhu la kushughulikia hali ya udhanaishi huu wa kidini na kujenga upya imani za vijana hawa kwenye dini zilizoasisiwa na mababu zao.

Tasnifu hii imegawanyika katika sura tano ambapo kila mojawake inaangzia masuala mahsusi kuhusu utafiti lengwa.Sura ya kwanza ilishughulikia utangulizi, usuli wa mada, tatizo na umuhimu wa utafiti.Pia,malengo na maswali ya utafiti yameshughulikiwa,msamiati uliotumika pamoja na upeo wa mipaka ya utafiti zilifafanuliwa kwenye sura hii ya kwanza. Katika sura ya pili,nadharia zilizoongoza utafiti huu zilifafanuliwa na pia mwauo wa maandishi ukaangaziwa kwa kina. Kwenye sura ya tatu,muundo wa utafiti,sampuli na uteuzi wake,mbinu na vifaa vya kukusanya data na maadili ya utafiti yaliangaziwa kwa kina.

Sura ya nne ilishughulikia uwasilishaji na uchambuzi wa data pale ambapo mtafiti alijishughulisha na udhanaishi wa kidini kwa vijana na athari zake. Kutokana na data iliyokusanywa,ilibainika kwamba kuna masuala nyeti yanayofanyika maabadani ambayo yamefanya vijana kukinai na dini kila uchao. Ilibainika kuwa baadhi ya waumini wanaotarajiwa kuwa kielelezo,wamejikita kwenye mipango ya kando na kufanya mapenzi nje ya ndoa. Wahubiri na wana wa watumishi wa Mungu wanaacha wachumba wao na kufanya mapenzi na wake na mabinti za wenyewe.

Mapenzi haya yanazaa matunda ya mimba zinazopatikana nje ya ndoa na baadaye kuvurunga ndoa za waumini hawa.Imebainika kuwa kuna mifarakano isiyoisha miongoni mwa madhehebu ya waumini. Mifarakano hii hufanyika hadharani huku viongozi wa kidini wakipatikana katikati yake. Kuna wale wanaozozania washirika huku wengine waking'ang'ania sehemu za kuezeka maabadi yao. Mizozo hii inafanya waumini wapigane hadharani na kuumizana bila kujali athari zake kwenye jamii inayowazunguka. Katika utafiti, imebainika kuwa baadhi ya viongozi wa dini wamekuwa wakitumia vibaya matoleo ya washirika wao na pia misaada inayotumwa kutoka ng'ambo kusaidia wenye mahitaji maalumu.Wengine wamekuwa wakitumia matoleo haya kwa



Mount Kenya University

majukumu yao ya kibinafsi na kujifaidi wao wenyewe. Mtafiti amebaini kuwa miaka ya hivi karibuni,maabadi yanazidi kufanywa kuwa mali ya familia. Imebainika kuwa viongozi wengi wanaoshika usukani kwenye mchakato mzima wa uongozi kwenye madhehebu mengi hutoka kwa familia moja na haswa ya wahubiri.Familia husika ndio huhubiri,huchukua sadaka na kuongoza ibada kwa jumla.

Vile vile,imebainika kuwa kuna biashara nyingi haramu zinazofanyika kwenye majengo ya maabadi mathalani biashara za dawa za kulevya pamoja na ulanguzi wa watoto.Biashara hizi haramu zinafanywa kwa jina la Mungu na kuongozwa na wale wanaotarajiwa kuwa kielelezo cha maadili mema kwa jamii nzima. Imebainika kuwa kuna ufisadi wa hali ya juu miongoni mwa viongozi wa kidini.

Baadhi ya Viongozi hawa wanaotarajiwa kuwa kielelezo kwa jamii ndio wanaotoa hongo ili kupendelewa kwa kesi zao mahakamani. Pia viongozi hawa wa kidini wanatumia vyeo walivyo navyo maabadani kujifaidi na kufaidi watoto wao kielimu badala ya kuauni watoto wa walala hoi. Utafiti huu umebaini dhahiri shahiri kuwa dini imekuwa ikitumika kama chombo cha kujitajirisha.Baadhi ya wahubiri wanamiliki ardhi na magari ya kifahari zilizogharamiwa na matoleo ya washirika. Viongozi hawa wa kidini pia wana akaunti kadhaa kwenye mabenki wanakohifadhi fedha za matumizi yao ya baadaye pamoja na jamii zao huku washirika wao wakizidi kumasikinika zaidi.

Isitoshe,imebainika kuwa viongozi wengi wa kidini wamekuwa wakiishi maisha ya anasa na starehe zinazogharamiwa na washirika wao. Hata sio muhari baadhi ya wahubiri kufanya miujiza bandia ili kuhini washirika wenye imani finyu ili wapate maisha ya starehe. Kuna wale wanaosafiri ng'ambo watakavyo,hula vyakula vya kifahari na huishi kwenye vyumba vya kifahari vilivyoezekwa kwenye mitaa ya kifahari.

Imebainika pia kuwa baadhi ya viongozi na waumini stadi wanahusishwa na mapepo,uganga na nguvu za giza kwa jumla.Baadhi yao wanalaumiwa kuwa na mapepo yanayosumbua

wanakijiji usiku,wanatupia watu mapepo yanayowafanya kuwa wendawazimu na pia wanajigeuza usiku wa shetani na kuzurura mitaani watu wakiwa usingizini. Pia baadhi ya waumini wanaposhuku uwezo wa Mungu wanatembelea waganga wa kienyeji usiku ili kuganguliwa.

Aidha,imebainika kuwa vitendo vya waumini wengi ni vya kinafiki tu. Hii ina maana kuwa kile wasemacho na kile wafanyacho vimebaidika kama ardhi na mbingu.Kukiwa na mwanga na kwenye kadamnasi ya watu watajifanya weupe kama pamba lakini usiku wa giza vitendo vyao vyafananishwa na vya Sodoma na Ngomora kama anavyosema Mhubiri Michael kwenye riwaya ya *Paradiso*.

Vile vile utafiti huu ulichanganua athari zinazotakana na udhanaishi wa kidini kwa vijana pale ambapo athari hizi zilijitokeza wazi kwenye riwaya teule. Athari hizo ni pamoja na vijana kuchoshwa na utaratibu wa ibada ambazo husheheni kelele nyingi na kuchukua muda mrefu. Hali hii huwachosha na wengi wao kukinaishwa na dini wangali kwenye miaka ya utotoni.

Pia kuna hali ya vijana kushuku uwezo wa Mungu kwani kulingana nao viongozi wengi wa kidini wanawalaghai washirika wao na kufanya makubwa kwa kudai kuwa wamewezeshwa na Mungu. Hali hii imefanya baadhi ya vijana kuamini kuwa kuna mambo kadhaa wanaweza wao wenyewe na kwao Mungu huingilia tu uwezo wao unapoingiwa na udhaifu tu. Athari nyingine ni kuwa baadhi ya vijana wamekataa kuokoa kwa madai kuwa hawaoni tofauti kati yao na wanaodai wameokoa kwani vitendo vya 'waliookoka' vimejawa na unafiki wa kila aina.

Unafiki wa viongozi wa kidini haswa wa kiume umewapelekea vijana wa kike kukataa kuolewa na wahubiri kwani wengi wao wanahusishwa na mipango ya kando nje ya ndoa. Vitendo hasi vya baadhi ya viongozi wa kidini umejaza vijana na moyo wa kudharau watumishi wa Mungu hadharani kwani hata wao wanafanya vituko vya aibu hadharani. Vijana hawana heshima tena kwa viongozi wa kidini ilivyokuwa kabla ya karne hii tunayo. Ongezeko la maadili telezi miongoni mwa baadhi ya viongozi wa kidini umechochea vijana kuzinduka na kuuliza maswali

moja kwa moja kuhusu imani na dini na yale wasiyoafikiana nayo. Vijana hawa hawaogopi tena kuuliza wasichokielewa vyema ili kufafanuliwa inavyofaa.

Baadhi ya vijana wanaopendekezwa kuendeleza kazi ya Mungu baada ya wazee wao kushuka ulingoni,wameanza kukataa kazi ya Mungu baada ya kugundua kuwa makuruhu mengi yanafanyika kwa jina la Mungu. Wametambua kuwa ingawa dini zote huhubiri haki na mema, yanayofanyika usiku wa giza yanaatua nyoyo za waja. Athari nyingine inayotikisa ulimwengu wa vijana ni kuwa baadhi yao wameacha kuhudhuria ibada kama ilivyoasisiwa na wavyele wao na badala yake wanajipa shughuli za kibinafsi siku zilizotengwa kwa shughuli hii muhimu kwa binadamu. Hii ni baada ya kupata mwanga kuwa ibada zenyewe zimekuwa zikitumiwa kwa minajili ya kunufaisha na kutajirisha baadhi ya viongozi wa kidini.

Hatimaye,imebainika kuwa baadhi ya vijana wamekuwa na mitindo hasi ya kutafuta miungu mingine na kujiingiza kwenye ibada zingine kinyume na mafundisho ya dini zao. Hii ni baada ya kukosa Imani na 'Mungu' wa miujiza ya Musa kwani baadhi ya wahubiri wamejikita kwenye miujiza bandia huku wakiwahadaa waumini wenye imani dhaifu.

Hitimisho la tasnifu hii limeshughulikiwa katika sura ya tano. Muhtasari wa kila mojawapo wa sura umetolewa katika sura hii yakiwemo matokeo ya utafiti yanayolingana na malengo ya utafiti huu. Hatimaye mapendekezo ya utafiti huu yametolewa kwenye sura hii ya tano.

Mount Kenya University

## 5.2 Mapendekezo ya Mtafiti

Kutokana na matokeo ya utafiti huu,yafuatayo ni baadhi ya mapendekezo ya utafiti zaidi unaoweza kuendelezwa siku za usoni.

Kwanza,suala hili la utafiti linaweza kushughulikiwa katika riwaya nyingine tofauti za waandishi tofauti na zilizotumiwa katika utafiti huu.

Pili,suala hili la utafiti linaweza kutafitiwa katika tanzu nyingine za fasihi ikiwa ni pamoja na tamthilia,hadithi fupi na hata ushairi.

Tatu,watafiti wa siku zijazo wanaweza kutumia nadharia nyingine tofauti na zilizotumika katika utafiti huu katika kulitafitia suala hili.

Nne,tafiti za usoni zinaweza kuangazia udhanaishi wa kidini kwa wanandoa katika riwaya teule za Kiswahili.

Tano,utafiti unaweza kuendelezwa kuhusu udhanaishi wa kidini kwa wasomi mbalimbali katika kazi za fasihi.

Sita,utafiti unaweza kuendelezwa kuhusu udhanaishi wa kidini kwa wanaume katika kazi teule za fasihi ya Kiswahili.

Hatimaye,mtafiti wa baadaye anaweza kulinganisha udhanaishi wa kidini kwa vijana wa kiume na wale wa kike katika kazi teule za fasihi ya Kiswahili.

Mount Kenya University

**5.3 Hitimisho**

Sura hii ya tano imeangazia muhtasari wa sehemu zote tano za utafiti,hitimisho la utafiti pamoja na mapendekezo ya mtafiti kwa wasomi na watafiti wa baadaye ambao wangekuwa na nia ya kushughulikia mada ya udhanaishi wa aina yoyote.Imebainika kuwa watu wa vitengo mbalimbali wakiwemo viongozi wa dini,maafisa wa serikali,mahakama,wazazi na walezi pamoja na jamii zilizoathirika zinapaswa kuwa mstari wa mbele kujifunga kibwebwe kukabiliana na udhanaishi wa kidini kwa vijana ili kujenga imani ya dini miongoni mwa vijana wa karne ya ishirini na moja.Vile vile,vijana wenyewe wana jukumu la kusaka madhehebu yaliyo ya ukweli na yaliyo tayari kutimiza matakwa yao ya kiroho bila hadaa na udanganyifu wa aina yoyote ile. Hii itasaidia kuijenga imani ya kidini inayofifia kwao kila uchao.

## MAREJELEO


Allen,G.(2000).*Intertextuality*.U.S.A and Canada:Routledge

Bennett,M.(2011).*Reassessing the Theatre of the Absurd*. New York:Palgrave Macmillan

Camus,A.(1953*).The Rebel*: Hamish Hamilton,Loudon.

------------(1961)*Resistance*,*Rebellion and Death*.Translated by Justin O'Brien.New York:Knopf

Cresswell,J.W.(2009).*Research Design*:*Qualitative,Quantitative and Mixed Methods Approaches*.Los Angeles:SAGE Publishers

Cruickshank,J.(1958).Albert Camus*:The literature of Revolt*: Oxford University press London

Esslin,M.(1974*).The Theartre of the Absurd*: Methien,London

Foulquie,P.(1947*).Existentialism*: Dennis Dobson ltd,London.

Freeman,E.(1971).*The Theatre of Albert Camus*.Methuen.London.

Green,N.N.(1960).Jean –Paul Sartre*: The existentialist Ethic*.The university of Michigan press U.S.A.

Habwe,J.(2000). *Maisha Kitendawili*.Nairobi.Jomo Kenyatta Foundation

-------- (2005).*Paradiso*.Nairobi;The Jomo Kenyatta Foundation.

Heinemann,F.H.(1958).*Existentialism and the Modern Predicament*.New York Harper & Brothers Publishers.

International Bible Society (1973). *Holy Bible*:New International Version.New York.

Katiba ya Kenya (2010).*Goverment Printers*.Nairobi

Kaufmann,W.(1956). *Existentialism From Dostoevsky to Sartre.*New York.Meridian Books Inc.

Kezilahabi,E.(1971). *Rosa Mistika*. Kenya Literature Bureau. Nairobi

-----------------(1974*) Kichwa Maji*.East African Publishing House.Nairobi.

---------------------(1981*).Dunia uwanja wa Fujo*. East African publications ltd. Arusha

--------------------(1974).*kichomi*.london;Heinemann Education Books (EA) ltd

King'ei, K.(1997*).Mwongozo wa Amezidi*. East African publishers,Nairobi

Kothari,R.C.(2004*). Research Methodology: Methods and Techniques*,New Delhi: New Age International (p) limited publishers.

Lepp,I. (1968*). Death and its mysteries. Burns and Dates*. London.

Lewis,A. (1962). *The Contemporary Theatre:* Crown Publishers,Inc. New York.

Macquarne,J. (1972). *Existentialism*: World Publishing Co.New York.

Magare,F(2002): "Uhakiki wa Tamthilia ya *Amezidi* Kama Kazi ya Kiubwege"Chuo Kikuu cha Nairobi.Tasnifu Ya M.A(Haijachapishwa)

Makoyo,M.S. (2014). ''A Critique of Christian Education for Self Reliance in Kenya i light of Existentialism''.Tasnifu ya Uzamili. Chuo Kikuu cha Nairobi.(Haijachapishwa)

Massamba,D.(.2002). *Historia ya Kiswahili*:*50BK hadi 1500BK*.Nairobi:Jomo Kenyatta Foundation.

Mbatia,M.(1997). *'Miongozo mipya katika uandishi wa Kazilahabi'* makala haya hayajapishwa.

Mbiti,J.(1969). .*African Religions and Philosophy*.London:Heinman Education Books Ltd.

Mohamed S.A. (1995*). Amezidi*. East African Educational publishers. Nairobi.

Mose,E.2005 ''*Taashira ya Kifo katika Tamthilia za* '*Mukwawa wa Uhehe'*, '*Amezidi'*, '*Kilio cha Haki' na* '*Visiki'* ''. Tasnifu ya Uzamili.Chuo Kikuu cha Kenyatta.(Haijachapishwa)

Mosoku,G.(2017) .State to Help Find Truce in SDA Church Conflict.*The Standard*,22nd January, 2017,p.23

Mugenda,O.&Mugenda,A.(2003)..Research Methods:Quantitative and Qualitative Approaches.Nairobi:Africa Center for Technology Studies(ACTS)Press.

Mungah,C.(1999). ''Dhana ya Maisha Katika Novela Mbili za Euphrase Kezilahabi:Nagona na Mzingile''Chuo Kikuu cha Nairobi.Tasnifu ya M.A(Haijachapishwa)

Mount Kenya University

Mulokozi,M,M.(1999). *Tenzi Tatu Za Kale* (*Fumo Liyongo*,Al-*Inkishafi*,*Mwanakupona*). Dar es Salaam. TUKI

Njogu,K. Na Chimera, R. (1999*). Ufundishaji wa Fasihi*: Nadharia na Mbinu. Nairobi: Jomo Kenyatta foundation.

Nkonge,G.(2006). " Athari za Udhanaishi katika *Kichwa Maji* na *Nguvu za Sala*" Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Nairobi( Haijachapishwa)

Nyamemba,(2012).'Uchanganuzi Linganishi wa jinsi waandishi katika *Tunu ya Ushairi* wanavyoshughulikia masuala ya vijana" Tasnifu ya Uzamili ,Chuo Kikuu cha Nairobi ( Haijachapishwa)

Onimus, J. (1970).*Albert camus and Christianity*; Gill and Macmillan, London

Roubiczek, P (1964*). Existentialism for and Against*. Cambridge University press. London

Rono,P. (2013). "*Uhakiki wa kimaudhui na kifani wa Kidagaa Kimemwozea* " Tasnifu ya Uzamili,Chuo Kikuu cha Nairobi ( Haijachapishwa)

Sartre,J.P.( 2007). Existeantialism is humanism. New Haven :Yale University Press .Original work published in 1945.

Senkoro,F(1982). *Fasihi*.Dares es Salaam:Press and Publicity Center

Sigmund,F. (1961) .*The Future of an illusion*. W.W Norton and Co.ltd. New york.

Tarantino,E.&Caruso,C(2009). .*Nonsense and Other Senses*:*Regulated Absurdity in Literature*. London:Cambridge Scholars Publishing.

Taylor,S(1984). *Iintroduction to Qualitative Research Methods*:*The Search for Meanings*.New York:John Wiley & Sons.

TUKI (2012*). Kamusi ya Kiswahili Sanifu* (Toleo la 3)Nairobi. Oxford University.

Wafula,R & Njogu,K.(2007): *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*.Nairobi:Jomo Kenyatta Foundation

Walibora,K .(.2012). *Kidagaa Kimemwozea*,Nairobi;Target Publication Limited

----------------(2006). *Kufa Kuzikana* .Nai robi;Target Publications

Wamitila,K(2003). *Kamusi ya Fasihi na Nadharia*.Nairobi Focus Publications

---------------. (2008). *Kazi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa fasihi*: Nairobi,Vide-Muwa Publishers.

Williams,R (1966*). Modern Tragedy*. Chatto & Windus Ltd,London

Mount Kenya University

**Kiambatisho I:Barua ya idhini ya Chuo.(ERC)**

Mount Kenya University

# Mount Kenya University

REF: **MKU/ISERC/3377**
TO: **MULI SOLOMON M.**

Date: 06 December 2023

REG: **MAKI/2020/64910**

Dear Sir/Madam,

**RE: ATHARI ZA UDHANAISHI WA KIDINI KWA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA PARADISO NA KIDAGAA KIMEMWOZEA**

This is to inform you that **Mount Kenya University** has reviewed and approved your above research proposal. Your application approval number is **2421.** The approval period is **06/12/2023 - 05/12/2024.**

This approval is subject to compliance with the following requirements;

i. Only approved documents including informed consents, study instruments, MTA will be used
ii. All changes including amendments, deviations and violations are submitted for review and approval by **Mount Kenya University**
iii. Death and life threatening problems and serious adverse events or unexpected adverse events whether related or unrelated to the study must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours of notification
iv. Any changes, anticipated or otherwise that may increase the risks or affect the safety or welfare of study participants and others or affect the integrity of the research must be reported to **Mount Kenya University** within 72 hours
v. Clearance for export of biological specimens must be obtained from relevant institutions
vi. Submission of a request for renewal of approval at least 60 days prior to expiry of the approval period. Attach a comprehensive progress report to support the renewal
vii. Submission of an executive summary report within 90 days upon completion of the study to **Mount Kenya University**

Yours sincerely,

The Chairman
Mount Kenya University
Ethics Review Committee
P. O. Box 342 - 0100, Thika

**Dr. Alfred Owino, PhD**
**Chairman, Mount Kenya University ISERC**

Main Campus, General Kago Road, P.O. Box 342-01000 Thika.
Cell: +254 709 153 000 / +254 709 153 200
Email: info@mku.ac.ke, Web: www.mku.ac.ke
Chartered and ISO 9001 : 2015 Certified Institution.
Unlocking Infinite Possibilities

**THE SCIENCE, TECHNOLOGY AND INNOVATION ACT, 2013 (Rev. 2014)**
Legal Notice No. 108: The Science, Technology and Innovation (Research Licensing) Regulations, 2014

**The National Commission for Science, Technology and Innovation**, hereafter referred to as the Commission, was the established under the Science, Technology and Innovation Act 2013 (Revised 2014) herein after referred to as the Act. The objective of the Commission shall be to regulate and assure quality in the science, technology and innovation sector and advise the Government in matters related thereto.

**CONDITIONS OF THE RESEARCH LICENSE**

1. The License is granted subject to provisions of the Constitution of Kenya, the Science, Technology and Innovation Act, and other relevant laws, policies and regulations. Accordingly, the licensee shall adhere to such procedures, standards, code of ethics and guidelines as may be prescribed by regulations made under the Act, or prescribed by provisions of International treaties of which Kenya is a signatory to
2. The research and its related activities as well as outcomes shall be beneficial to the country and shall not in any way;
   i. Endanger national security
   ii. Adversely affect the lives of Kenyans
   iii. Be in contravention of Kenya's international obligations including Biological Weapons Convention (BWC), Comprehensive Nuclear-Test-Ban Treaty Organization (CTBTO), Chemical, Biological, Radiological and Nuclear (CBRN).
   iv. Result in exploitation of intellectual property rights of communities in Kenya
   v. Adversely affect the environment
   vi. Adversely affect the rights of communities
   vii. Endanger public safety and national cohesion
   viii. Plagiarize someone else's work
3. The License is valid for the proposed research, location and specified period.
4. The license any rights thereunder are non-transferable
5. The Commission reserves the right to cancel the research at any time during the research period if in the opinion of the Commission the research is not implemented in conformity with the provisions of the Act or any other written law.
6. The Licensee shall inform the relevant County Director of Education, County Commissioner and County Governor before commencement of the research.
7. Excavation, filming, movement, and collection of specimens are subject to further necessary clearance from relevant Government Agencies.
8. The License does not give authority to transfer research materials.
9. The Commission may monitor and evaluate the licensed research project for the purpose of assessing and evaluating compliance with the conditions of the License.
10. The Licensee shall submit one hard copy, and upload a soft copy of their final report (thesis) onto a platform designated by the Commission within one year of completion of the research.
11. The Commission reserves the right to modify the conditions of the License including cancellation without prior notice.
12. Research, findings and information regarding research systems shall be stored or disseminated, utilized or applied in such a manner as may be prescribed by the Commission from time to time.
13. The Licensee shall disclose to the Commission, the relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee, and the relevant national agencies any inventions and discoveries that are of National strategic importance.
14. The Commission shall have powers to acquire from any person the right in, or to, any scientific innovation, invention or patent of strategic importance to the country.
15. Relevant Institutional Scientific and Ethical Review Committee shall monitor and evaluate the research periodically, and make a report of its findings to the Commission for necessary action.

National Commission for Science, Technology and
Innovation(NACOSTI),
Off Waiyaki Way, Upper Kabete,
P. O. Box 30623 - 00100 Nairobi, KENYA
Telephone: 020 4007000, 0713788787, 0735404245
E-mail: dg@nacosti.go.ke
Website: www.nacosti.go.ke

## Kiambatanisho II: Barua ya Idhini(NACOSTI)

National Commission for Science, Technology and Innovation -

REPUBLIC OF KENYA

**NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION**

Ref No: **571959**

Date of Issue: **24/January/2024**

**RESEARCH LICENSE**



**This is to Certify that Mr.. SOLOMON Mbio MULI of Mount Kenya University, has been licensed to conduct research as per the provision of the Science, Technology and Innovation Act, 2013 (Rev.2014) in Kiambu on the topic: ATHARI ZA UDHANAISHI WA KIDINI KWA VIJANA KATIKA RIWAYA ZA PARADISO NA KIDAGAA KIMEMWOZEA for the period ending : 24/January/2025.**

License No: **NACOSTI/P/24/32670**

**571959**

Applicant Identification Number

Director General
NATIONAL COMMISSION FOR SCIENCE,TECHNOLOGY & INNOVATION

Verification QR Code

NOTE: This is a computer generated License. To verify the authenticity of this document, Scan the QR Code using QR scanner application.

**See overleaf for conditions**